# MATATIZO KWENYE UJUMBE KATIKA KALIMANI ZA MAHUBIRI YA KIDINI MJINI BONDO.

OWALA, S.O

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi.**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON.**

**FEBRUARI 2006.**

Eger241282

## UNGAMO NA IDHINI.

### UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote kile.

Owala Silas Odhiambo

Sahihi..... Tarehe 02/05/06

### IDHINI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na chuo kikuu.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

Dkt. James Onyango Ogola

Sahihi..... Tarehe 02/05/06

© **HATILINZI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kuiga tasnifu hii kwa mfumo wowote ule bila ya idhini ya mwandishi au/na Chuo Kikuu Cha Egerton.

## TABARUKU

Kazi hii namtabaruku babangu mzazi -Meshack Owala ambaye weledi wake wa Kiswahili ulinisisimua kila mara alipoizungumza lugha hiyo.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt.Chai pamoja na Dkt.Onyango ambao walinipa msaada mkubwa sana na hasa kwa kuwepo kila mara nilipowahitaji. Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wengine katika idara kama vile Dkt.Beja, mwalimu Gwachi na wengine katika Idara ya Lugha na Isimu ambao maelekezo yao yaliniwezesha kuifikisha kazi hii mahali ilipo.

Pili ningependa kuwashukuru wenzangu wa darasani Sangolo Alubaka na Rotich Kibet ambao walinisaidia sana kimawazo ili kazi hii iweze kujengeka. Maoni yao yalinisaidia sana na kuniwezesha kuwa na mtazamo mpana kuhusu utafiti huu. Tatu ni kwa wanafunzi wangu katika Chuo Cha Ualimu Cha Bondo ambao walinisaidia kwa kupitia baadhi ya tunukuzi na kuweza kugundua matatizo hapa na pale.

Siwezi kuisahau jamaa yangu, mke wangu mpenzi Jane Ongachi pamoja na wanangu Oscar Owala na Gift Owala ambao kujinyima kwao kihali na kimali kuliniwezesha kuikamilisha kazi hii. Rafiki zangu wengi walinisaidia kwa kunihimiza kila nilipoonyesha dalili za kukata tamaa. Sitamsahau Bi.Lucy Barimbui wa Chama cha Walimu Nairobi kwa kipawa hicho adimu cha kuhimiza.

Shukrani zangu zingine ziwaendee wapiga chapa wa Katinas Bondo.Roseline Akinyi, Carren Chek na Elma Akumu ambao walinifanyia kazi kwa kujitolea hata wakati uchovu ulinifanya nionyeshe hali ya kutokuwa na uvumilivu.

Mwisho ni kwa wahadhiri wenzangu Bwana James Majiwa na Bwana Joseph Amuke ambao nilifaidika kutokana na kompiuta zao. Ingawa siwezi kumtaja kila mtu kwa jina, kuna watu kadha wa kadha ambao nilifaidika kutokana na msaada wao.Nawashukuru wote na Mungu awabariki.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ukalimani katika mikutano ya kidini na hasa kama ujumbe uliowasilishwa katika lugha lengwa ni uleule uliokusudiwa katika lugha chanzi. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza ukalimani kutoka Kiingereza hadi Kiluo na Kiluo hadi Kiswahili ili kubainisha visababishi vya matatizo katika ujumbe kwenye kalimani. Utafiti huu ulizingatia Nadharia ya Nida ambayo mbali na kueleza maana ya tafsiri, inazungumzia umuhimu wa mazingira na utamaduni katika tafsiri na pia sifa zinazomfaa mtu anayetaka kufanya kazi ya tafsiri. Deta ilikuwa tunukuzi za mahubiri na ukalimani wake na maoni ya hadhira kwenye hojaji.

Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa watafiti wa kalimani hasa katika upande wa mbinu na nadharia. Ulinganishi wa lugha zinazohusika utabainisha tofauti za kimiundo za lugha husika. Pia mianya itajitokeza ya kufanyia utafiti zaidi katika nyanja hii ya ukalimani.Tumewasilisha kazi hii katika sura tano. Sura ya kwanza ni Ujenzi wa Utafiti.Sura ya pili ina Mapitio ya Maandishi pamoja na Msingi wa Nadharia. Katika sura ya tatu tumeonyesha mbinu tulizotumia kufanyia utafiti. Sura ya nne ina Matokeo ya Uchunguzi na hatimaye katika sura ya tano tumetoa Muhtasari kwa ujumla, Hitimisho na Mapendekezo.

## YALIYOMO

UNGAMO----------(ii)

HATILINZI----------(iii)

IKISIRI----------(iv)

SHUKRANI----------(v)

TABARUKU----------(vi)

YALIYOMO----------(vii)

SURA YA KWANZA:UTANGULIZI----------1

1.1 Utangulizi----------1

1.2 Usuli wa Mada----------1

1.3 Mada ya Utafiti----------2

1.4 Madhumuni ya Utafiti----------2

1.5 Nadharia Tete za Utafiti----------2

1.6 Umuhimu wa Utafiti----------2

1.7 Upeo wa Utafiti----------3

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI----------5

2.1 Utangulizi----------5

2.1.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti----------5

2.1.2 Maana ya Ukalimani----------5

2.1.3 Aina za Ukalimani----------7

2.1.4 Isimu katika Ukalimani----------8

2.1.5 Utamaduni na Mazingira katika Ukalimani----------10

2.1.6 Mkalimani na Mwegemeo wa Mkalimani----------11

2.2 Msingi wa Nadharia----------13

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI----------16

3.1 Utangulizi----------16

3.2 Utaratibu wa Utafiti----------16

3.3 Uteuzi wa Sampuli ----------16

3.4 Vifaa vya Ukusanyaji Deta----------17

3.5 Ukusanyaji Deta----------17

3.6 Uchanganuzi wa Deta ----------18

3.7 Matatizo yaliyokumba Utafiti----------18

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DETA ----------20

4.1 Utangulizi ----------20

4.2 Maoni ya Hadhira----------20

4.3 Wakalimani----------22

4.4 Matatizo yaliyojitokeza katika Ukalimani----------27

4.4.1 Utangulizi----------27

4.4.2 Matatizo ya Kileksia----------29

4.4.3 Matatizo Anuwai----------42

4.4.4Matatizo ya Kisintaksia----------55

4.4.5Matatizo ya Kimazingira na Kitamaduni----------57

4.4.6 Matatizo ya Lafudhi ya Mhubiri----------58

4.4.7 Matatizi ya Kasi ya Mahubiri----------58

SURA YA TANO : MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO----------59

5.1 Utangulizi ----------59

5.2.1 Muhtasari----------59

5.4. Mapendekezo----------61

MAREJELEO ----------62

VIAMBATISHO----------66

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa maelezo kuhusu msingi wa mada yetu. Vilevile tumeeleza utafiti huu ulikuwa na madhumuni gani kwa kubainisha malengo ya utafiti na nadharia tete ambazo ziliongoza utafiti wenyewe. Mwisho tumeeleza natija ya utafiti na upeo wake.

## 1.2 Usuli wa Mada.

Utafiti huu ulihusu ukalimani katika mikutano ya kidini ya Kikristo mjini Bondo.Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la watu mjini Bondo. Baadhi ya watu hao hawaelewi lugha ya Kiluo ambayo ndiyo lugha asilia ya wenyeji wa Bondo na vitongoji vyake. Jambo hilo limeleta changamoto kwa viongozi wa kidini ya kutafuta njia za kuwasiliana na watu wote wanaohudhuria mikutano ya kidini ya Kikristo mjini Bondo. Ili kutosheleza mahitaji ya kiroho ya watu wasioelewa lugha ya Kiluo imewabidi viongozi wa kidini kutumia ukalimani kuwasiliana na waumini wa makanisa yao.

Ukalimani hutekeleza jukumu muhimu katika ulimwengu wa sasa. Jambo hili limesababishwa na mambo mengi yakiwemo teknolojia ya mawasiliano usafiri ulioimarika na uhamiaji kutoka mashambani hadi mijini kwa sababu za kiuchumi na nyinginezo. Maingiliano yanayotokana na mambo hayo yanawafanya watu wanaozungumza lugha tofauti kushirikiana katika nyanja mbalimbali ikiwemo dini. Hali hii inaonekana hasa katika miji nchini Kenya ambayo huwa na watu wa makabila mbalimbali. Kutokana na hayo viongozi wa kidini ya Kikristo wametambua ukalimani kuwa chombo muhimu kinachowawezesha kuwasiliana na waumini wao ambao huwa watu wanaozungumza lugha tofauti.

Wakalimani wanatarajiwa kuhawilisha habari kutoka lugha moja hadi lugha nyingine papo kwa hapo. Udharura wa ukalimani humtwisha mkalimani jukumu kubwa sawa na mhubiri. Iwapo ujumbe una matatizo, lawama zitalimbikiziwa yeye mkalimani. Yeye ni kiungo muhimu kati ya mhubiri na hadhira yake.Mkalimani asipofanya kazi yake vizuri, mhubiri naye hatakuwa amewasiliana na hadhira.

Kalimani huzua matatizo mengi hasa ikiwa tamaduni na mazingira ya lugha chanzi ni tofauti na zile za lugha lengwa na vile vile ikiwa mkalimani hajapata mafunzo na matayarisho yafaayo . Licha ya hayo ukalimani bado unawezekana.

Mtafiti alichunguza ukalimani katika baadhi ya mikutano ya kidini katika mji wa Bondo ambapo lugha za Kiingereza na Kiluo zilitumiwa huku wakalimani wakitafsiri katika lugha ya Kiluo na Kiswahili katika usanjari huo.

### 1.3 Mada ya Utafiti

Ukalimani hutekeleza jukumu kubwa katika mikutano ya kidini ambayo waumini wanazungumza lugha tofauti. Hata hivyo baadhi ya wakalimani wana matatizo katika kukalimani ujumbe wa mhubiri na kwa hiyo kuna haja ya kuchunguza kiini cha matatizo hayo.

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo:-

i. Kucunguza matatizo ya ufasiri katika kalimani za kidini mjini Bondo.
ii. Kubainisha kiini cha kimazingira na kitamaduni kinachosababisha matatizo hayo.
iii. Kutathmini tajriba na mafunzo ya wakalimani wa kidini yanayohusiana na kazi ya ukalimani.

### 1.5 Nadharia Tete za Utafiti

i. Wakalimani katika mikutano ya kidini ya Kikristo mjini Bondo wana matatizo katika kufasiri ujumbe wa lugha chanzi.
ii. Kiini cha matatizo katika ukalimani katika mikutano ya kidini mjini Bondo hutokana na tofauti za kimazingira na kitamaduni kati ya lugha zinazotafsiriwa na lugha lengwa.
iii. Wakalimani katika mikutano ya kidini mjini Bondo hawajapata mafunzo maalum kuhusu kazi hiyo.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti huu

Ukalimani ni muhimu sana katika kufanikisha mawasiliano katika jamii na hasa zile jamii zenye watu wanaozungumza lugha tofauti.

Umuhimu wake hujitokeza zaidi katika mikutano ya hadhara katika maeneo ya miji.Mikutano ya kidini ni kati ya mikutano hiyo ya hadhara.Kuna haja ya kuchunguza maswala yanayohusu lugha hususan ukalimani katika mikutano hiyo ili kuweza kutoa mapendekezo yanayoweza kuboresha mawasiliano katika mikutano hiyo. Jambo hili litawanufaisha viongozi wa kidini hasa ikiwa watagundua kuwa wakalimani wao wana matatizo.

Katika mikutano kadhaa ya kidini tumesikia wakalimani wakifasiri visivyo ujumbe wa lugha chanzi. Jambo hili limeonekana katika runinga, redio na miongoni mwa wahuburi wa mitaani.

Ingawa utafiti huu ulifanywa mjini Bondo, matokeo ya utafiti huu yatayafaidi maeneo mengine nchini Kenya.Pamoja na hayo huenda ukatoa kichochezi miongoni mwa wanaisimu kuchunguza ukalimani katika mikutano ya kidini na nyanja zingine ndani na nje ya nchi ya Kenya kwa minajili ya kuboresha kalimani hizo. Uchunguzi kama huo mbali na kuchangia kuzua mbinu zifaazo za kufanya tafiti za aina hii pia unaweza kufungua maeneo mengine ya kufanyia utafiti hasa yale yanayohusu ukalimani. Nadharia zilizopo ambazo nyingi zinahusu tafsiri za matini andishi pia zinaweza kuangaziwa ili kuona ni zipi zinazofaa kutumiwa kufanyia utafiti kama huu. Mbali na hayo wanaisimu wanaweza kufaidika kutokana na ulinganishi utakaofanyiwa lugha zinazohusika ili kuelewa tofauti za kimuundo katika lugha hizo.Utafiti huu kwa hiyo utakuwa mchango katika uwanja ambao haujashughulikiwa na watu wengi.

**1.7 Upeo wa utafiti.**

Kuna mambo kadha wa kadha ambayo huweza kusababisha matatizo ya kubadilisha maana kutoka lugha moja hadi lugha nyingine , baadhi ya mambo haya ni :- .

- Tofauti za kitamaduni katika jozi za lugha ambazo husababisha ukosefu wa visawe katika lugha lengwa.
- Tofauti za kisemantiki (husababisha matatizo katika Uteuzi wa Kimantiki *(collocation)*
- Tofauti za kisintaksia.

Katika utafiti huu tulichunguza tunukuzi za ujumbe ambao tayari umebadilishwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiluo na Kiluo hadi Kiswahili. Lugha hizo ziliteuliwa kwa sababu mbili.Sababu ya kwanza ni kwamba maswala ambayo yanachunguzwa ni maswala ya kiisimu.Maswala haya ya kiisimu ni karibu sawa katika jozi zozote za lugha.

Ikiwa utafiti huu ungeradidiwa kwa kutumia lugha zingine hayo maswala ya kimsingi ya kiisimu bado yangebakia sawa. Sababu ya pili ni kwamba katika eneo ambalo utafiti huu ulifanywa yaani mjini Bondo, hizo ndizo lugha ambazo hutumiwa sana katika mikutano ya hadhara ya kidini.

Tuliangazia sehemu zote ambazo zilionekana kwamba zinaleta matatizo katika kuuelewa ujumbe uliokalimaniwa. Lugha zitakazochunguzwa katika utafiti huu ni zile ambazo zinaonyesha tofauti, mathalani Kiluo-Kiingereza na Kiluo –Kiswahili. Katika ukalimani kunao uhusiano baina ya lugha chanzi na lugha pokezi. Uhusiano huo hujidhihirisha hasa katika muundo, mtindo, ngeli na hata nyakati am njeo. Uhusiano huu ni wa aina mbili: -

1. Ule unaotoa maana ya juujuu
2. Ule unaotoa maana kulingana na muktadha fulani.

Katika ukalimani wa juujuu mkalimani hazingatii kiini cha ujumbe bali huzingatia neno kwa neno. Katika ukalimani wa kimuktadha mkalimani anazingatia maana ya vifungu vizima. Juu ya hayo ni muhimu kutaja kwamba katika dini ubunifu unakubaliwa tu katika kiwango fulani. Kiwango hicho ni kile ambacho hakibadili kimsingi dhana zilizomo katikadini hiyo. Vilevile kubadilisha maana ya usemi kwa kutia chumvi nyingi mno hakukubaliki.Maswala ya kiroho huwa na uhifadhina mwingi hivi kwamba ubunifu mwingi huchukuliwa kama mzaha, jambo ambalo halikubaliki. Katika utafiti huu, kutia chumvi au ubunifu ambao huonekana kubadilisha misingi ya imani ya dini ya Kikristo utachukuliwa kama tatizo. Ubunifu ambao hufanikisha mawasiliano bila kubadilisha msingi wa imani ya Kikristo itachukuliwa kwamba ni sawa.

Tulitumia vipengele vilivyotajwa hapo juu kutathmini ubora wake kwa kulinganisha yaliyosemwa katika lugha chanzi na yalivyotafsiriwa katika lugha lengwa. Tulichunguza matatizo katika kalimani hizo na kujaribu kubainisha chanzo chake.Utafiti huu ulijikita katika mikutano ya hadhara ya kidini mjini Bondo pekee.

## SURA YA PILI
## MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia maoni ya waandishi mbalimbali ambao wameandika juu ya uhawilishaji wa ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine. Tumeonyesha ni kwa jinsi gani maandishi hayo yanavyohusiana na utafiti huu. Katika kuangalia kazi hizo tumezingatia mada mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu.

### 2.1.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti.

Katika mapitio ya maandishi na tafiti mbali mbali kuhusu swala la ukalimani katika mikutano ya kidini mjini Bondo, hakuna yoyote yaliyopatikana yanayohusiana moja kwa moja na mada hii. Hii ni kwa sababu hakuna utafiti uliofanywa juu ya mada hii katika eneo hili. Pia maandishi mengi kuhusu uhamishaji wa maana kutoka lugha moja hadi nyingine yalikuwa ni ya tafsiri ambayo aghalabu huhusu zaidi matini andikwa badala ya ukalimani. Hata hivyo dhana hizo mbili, tafsiri na ukalimani zina uhusiano mkubwa. Kwa hiyo tulitumia baadhi ya maoni ya watafsiri na kuyahusisha na matatizo yanayotokea katika ukalimani.

### 2.1.2 Maana ya Ukalimani

Maana ya ukalimani ina uhusiano mkubwa sana na maana ya tafsiri. Kwa sababu hii tutazingatia maoni ya waandishi mbalimbali kuhusu tafsiri na hatimaye kuonyesha maoni hayo yanahusianaje na ukalimani na vilevile utafiti huu.

Cremona na Mallia (2001) ambao ni wataalam wa ukalimani katika mikutano ya kimataifa wanatoa maelezo yanayoonyesha tofauti kati ya mfasiri na mkalimani. Wao wamesema kwamba mtafsiri hufanya kazi peke yake akiwa na karatasi pamoja na matini. Wao huiunda upya matini hiyo sawa na mtunzi wa pili kwa kuelewa na kuumba upya stadi za mwandishi asilia. Mkalimani kwa upande mwingine, hafanyi kazi katika hali ya upweke. Yeye hufanya kazi pamoja na mnenaji ambaye wakati mwingine hufafanua mada yake na kueleza fikira zake moja kwa moja bila kumpa mkalimani wakati wa kutoa ufafanuzi upya au kutafuta vifasiri vifaavyo. Mkalimani, pia, huwa na hadhira ambayo humsikiza sawia na yule mnenaji. Kwa vile muda kati ya tamko la mnenaji na la mkalimani huwa mfupi sana. Jambo hilo huleta uwezekano wa mkalimani asiye makini kutumia maneno yasiyofaa ili kuepuka kusubirisha

hadhira yake. Utumizi huu wa maneno yasiyofaa ulichunguzwa katika utafiti huu.Lengo lilikuwa ni kubainisha kama ukalimani una maneno mengi yasiyowakilisha dhana kama ilivyo katika lugha chanzi. Kigezo hicho kilitumiwa kuamua kiwango cha matatizo katika ujumbe.Ingawa maoni hayo yana uhusiano mkubwa na utafiti huu,kuna tofauti kidogo. Wao walikuwa wakiandika kuhusiana na ukalimani unaofanywa katika nyanja ya kidiplomasia. Katika muktadha huo wakalimani huwa watu waliohitimu katika kazi hiyo na kuteuliwa kwa makini. Katika utafiti wetu walae wanaokalimani ni watu ambao hawajapata mafunzo ya aina hiyo. Pia,wengi ni watu waliojitolea kufanya kazi hiyo.

T.U.K.I(1990)-"Tafsiri ni habari iliyohamishwa kutoka lugha moja hadi lugha nyingine" Maoni haya yanatoa maelezo ya kimsingi tu bila kueleza mengi kuhusu tafsiri. Maoni hayo yanaelekea kuchukulia kwamba swala la tafsiri ni rahisi tu na kwamba hata hiyo habari iliyohamishwa haina haja kuchunguzwa kujua kama imehamishwa vyema au hapana. Mbali na hayo, maelezo hayo yanazungumzia zao la mchakato wa tafsiri na kupuuza mchakato wenyewe.

Catford (1965)- anasema kwamba kufasiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi ya lugha chanzi na kuweka badala yake mawazo yanayolingana kutoka lugha nyingine (lugha lengwa). Maoni hayo ya Catford yanaonyesha tahadhari zaidi. Ni bayana kwamba mwandishi huyo anatambua kwamba mambo yanayofasiriwa hayawezi kuwa sawa kabisa katika lugha lengwa na yale yaliyomo katika lugha chanzi. Hii ndiyo sababu anaingiza swala la ulinganishi katika maelezo ya tafsiri. Hapa Catford anazungumzia tafsiri ambayo humpa matafsiri nafasi ya kufanya huo ulinganishi. Katika utafiti wetu ambao unahusu ukalimani, nafasi kama hiyo haitakuwepo kwa sababu ya uhalisia wa mambo. Huwa hakuna muda wa kutosha wa kufikiria na kufanya ulinganishi kama ule ambao Catford anazungumzia hapo.

Nida (1964) Anaeleza tafsiri kuwa ni kuwasilisha katika lugha lengwa ujumbe wa lugha chanzi kwa maana iliyo karibu iwezekanavyo na pia kwa mtindo uliokaribu na vile ujumbe ulivyo katika lugha chanzi. Ukalimani vilevile hutumia msingi huuhuu tofauti ni kwamba ukalimani hufanywa papo kwa hapo ilhali tafsiri ni katika matini,lakini dhana ya kuhamisha maana ni ile ile

Ingawa utafiti huu haushughulikii tafsiri, maoni ya waandishi hao wawili yana umuhimu hivi kwamba ukalimani pia ni uhamishaji wa habari kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Kama ilivyo katika tafsiri,katika ukalimani kuna lugha chanzi na lugha lengwa au lugha pokezi.

Kama ilivyo katika tafsiri,mkalimani huchukua mawazo yaliyo katika lugha chanzi na kuweka badala yake mawazo yaliyolingana nayo katika lugha pokezi.

Swala la ulinganishi ni muhimu hapa kwa sababu ni vigumu kupata lugha mbili ambazo hulingana reale kwa ya pili. Tutazingatia jambo hili katika utafiti wetu kwa kutoshikilia kwamba lazima ukalimani uwe sawa kabisa na mawazo kama yalivyo katika lugha inayokalimaniwa.Tutachukulia tu kwamba kuna tatizo ikiwa mkalimani atatumia neno au maneno ambayo yanasababisha matatizo yanayofanya dhana inayohusika kutomfikia mpokezi. Vilevile tutachukulia kuwa kuna tatizo iwapo maneno ya mkalimani yatabadilisha maana inayojitokeza katika ujumbe asilia.

**2.1.3 Aina za Ukalimani.**

Ukalimani kama tafsiri unaweza kuwa wa moja kwa moja au ukalimani huru. Katika baadhi ya sehemu za dunia kama vile Uchina, wao husisitiza ukalimani wa moja kwa moja.Katika sehemu zingine za ulimwengu, ukalimani wa moja kwa moja ni nadra sana isipokuwa katika majina-hii ni kwa sababu tofauti za kiisimu haziruhusu tafsiri za moja kwa moja na hasa ikiwa lugha husika ni za jamii lugha tofauti kama vile Kiingereza na Kiluo.
Katika utafiti huu kwa mfano, lugha zinazohusika yaani Kiluo, Kiingereza na Kiswahili zinatoka katika jamii lugha tofauti-Kiluo ni kinilotiki, Kiswahili ni Kibantu na Kiingereza ni Kikaukasia. Hii ina maana kwamba tafsiri za moja kwa moja zinaweza kusababisha baadhi ya matatizo ambayo yanazungumziwa katika utafiti huu.

Mwansoko (1996) anaelekea kukubaliana na Nida kwa kukashifu tafsiri za neno kwa neno kwa kusema kwamba tafsiri aina hii huzingatia maana za kimsingi za maneno bila kujali muktadha. Mara nyingi haitowi kwa wangavu maana inayokusudiwa kwa sababu nahau na misemo inayohusiana na utamaduni hufasiriwa kisisisi. Maoni hayo ya Nida pamoja na Mwansoko ni muhimu sana katika ukalimani. Mkalimani huwajibika kufanya maamuzi ya haraka kuhusu maana ya yale yanayosemwa badala ya kuzingatia tu maneno ya mnenaji. Utafiti huu ulichunguza uwezo wa mkalimani kufanya hivyo.Tunajua kwamba kwa vile mkalimani huwa hana muda wa kutosha kufikiria yale ambayo mhubiri amesema,kuna jaribio kubwa sana la kukalimani maneno ya mhubiri moja kwa moja bila kuzingatia muktadha way ale ambayo yamesemwa na mhubiri.

Kwa vile mkalimami hana muda mrefu wa kufikiria yale yaliyosemwa na mhubiri, kuna uwezekano wa mkalimani kupuuza ujumbe wenyewe na kujikita katika kutafsiri maneno ya mhubiri tu. Hali hiyo inaweza kusababisha kutingwa kwa mawasiliano kati ya mhubiri na hadhira yake. Uwezo wa mkalimani wa kufanya maamuzi ya haraka kuhusu maana ya yale yanayosemwa badala ya kuzingatia tu maneno ya mhubiri ulitumiwa kama kigezo cha kuamua kama ujumbe uliokalimaniwa una matatizo au la.

### 2.1.4 Isimu katika Ukalimani

Ukalimani ni kazi inayofanyiwa lugha.Ni mtindo wa kubadilisha mawazo katika lugha moja na mawazo katika lugha nyingine –kutafuta mfanano wa maana katika ile lugha nyingine.Isimu hutokana na tabia za lugha zinazodhihirika katika viwango mbalimbali. Hivi viwango ni kama vile: fonolojia,leksia,sintaksia na kiwango cha semantiki. Lugha zote za ulimwengu huchunguzwa katika viwango hivyo vinne. Kuna lugha zingine ambazo zinaonyesha mfanano katika viwango hivyo hasa, lugha zinazotoka katika jamii lugha moja ilhali zingine zinaonyesha tofauti kubwa. Katika utafiti huu viwango vya leksia na sintaksia vitazingatiwa ili kubainisha vile viwango hivyo vya lugha vinavyoathiri maana na kusababisha matatizo katika kukalimani kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa.

Nida (2002) anasisitiza kwamba ni muhimu kuzingatia visawe amilifu katika tafsiri. Kwa hiyo, tafsiri ijikite katika maana badala ya mfanano wa kirasimu ambao husababisha matatizo kimaana. Watu wana haja ya kujua maana ya yale yanayosemwa na si tafsiri ya maneno yanayotamkwa. Ni rahisi zaidi kutafsiri neno kwa neno lakini maneno hayo huenda yasiwe na maana iliyokusudiwa. Hii ni kwa sababu maneno huwa na maana tofauti kwa kutegemea muktadha. Watafsiri kadhaa huishilia kuabudu maneno bila kufanya matini hiyo kuweza kueleweka. Alitoa mfano wa *Hallowed be thy name* katika sala ya bwana ya Wakristo ambayo anasema hata Waingereza wana matatizo kueleza maana yake. Swala la muktadha ni muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu katika lugha ya Kiluo neno moja linaweza kuwa na maana nyingi kwa kutegemea muktadha ilimotumiwa. Ikiwa mkalimani ambaye anatafsiri kutoka lugha ya Kiluo hadi lugha nyingine si makini,huenda uteuzi wa kimantiki ukamtatiza.Hii ni kwa sababu lugha ya Kiluo huwa na maneno mengine ambayo huwa na maana zidi ya moja, na uteuzi wa neon moja badala ya jingine hutegemea muktadha.

Aiwei Shi (2004) anasema kwamba katika tafsiri au ukalimani kuna haja ya urekebishaji wa ujumbe katika lugha lengwa. Katika urekebishaji, mabadiliko hufanywa ili kuleta uwiano kati ya matini lengwa na dhana katika matini chanzi. Tafsiri sio tu mabadiliko ya kiisimu kati ya lugha bali hujumuisha urekebishaji katika kiwango cha utamaduni, siasa, na ujumi.
Urekebishaji ni lazima iwapo thamani ya ujumbe chanzi itahifadhiwa. Kwa maoni ya watafsiri wa kimagharibi, 'tafsiri ni kama mwanamke, kama ni mwaminifu, si mrembo, kama ni mrembo si mwaminifu'.Maoni haya hutokana na nadharia mbili zinazokinzana za tafsiri-ile inayozingatia ujumbe chanzi na ile inayozingatia ujumbe lengwa. Tafsiri ilyozingatia ujumbe chanzi ilichukuliwa kuwa bora kwa muda mrefu.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, hali hii imeanza kubadilika na ujumbe lengwa kutiliwa mkazo. Katika mikutano ya kidini kuna haja ya kusisitiza kwamba mkalimani ajibidiishe kuhakikisha kuwa wapokeaji wa ujumbe wananufaika na ukalimani wake badala ya kuwania kutafsiri tu maneno kutoka kwa lugha chanzi. Wanaisimu wengi wanakubaliana kwamba ikiwa kuna sababu za kiisimu au za kitamaduni ambazo hufanya neno fulani kutoweza kufasirika, ni bora kufanya urekebishaji ufaao badala ya kulitafsiri neno kwa neno. Mkalimani kwa hiyo atatarajiwa kutoa maelezo yatakayowafanya wale wanaomsikiza kupata kwa karibu iwezekanavyo dhana inayoelezwa. Tulichukulia kalimani zilizozingatia ujumbe lengwa badala ya ujumbe chanzi kuwa ni bora zaidi. Kwa maoni yetu mbali na kuwasilisha yale ambayo mhubiri amesema,ilikuwa muhimu vilevile kuhakikisha kwamba wale wanaolengwa wamepata ujumbe kwa namna inavyoeleweka katika lugha lengwa.

Fram-Cohen(1985) anasema kuwa dhana kwamba maneno yanayokalimaniwa au kutafsiriwa si lazima yawe visawe inaweza kudhihirishwa kwa kuonyesha kuwa neno moja linaweza kuwa na maana zaidi ya moja katika lugha chanzi -kwa mfano 'paa' katika Kiswahili. Kila maana huwakilisha dhana tofauti katika lugha chanzi ilhali katika lugha lengwa huenda dhana hizo zikawakilishwa na maneno tofauti. Ili kukalimani sawasawa mkalimani lazima atambue kuwa dhana inayozungumziwa ina maana gani katika lugha chanzi. Ikiwa mkalimani atashindwa kubainisha kati ya dhana tofauti katika lugha chanzi, huenda akachagua neno lililo na maana tofauti katika lugha lengwa. Tatizo hili lilitokea katika kutafsiri Biblia katika lugha ya Kilatini kutoka kwa lugha ya Kihibrania. Kuna sehemu inayosema *"and rays glowed from Moses' face"*. Katika lugha ya Kihibrania, *rays* na *horns* ni *karnayim.* Mtafsiri alichagua neno la Kilatini lililo na maana ya *horns* na kwa hiyo kutafsiri sehemu hiyo kuwa *"and horns grew on*

*Moses' head*". Mfano huo unaonyesha jinsi matatizo yanaweza kutokea wakati wa ukalimani wa ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine.Matatizo kama haya yanaweza kuwa mbaya zaidi katika ukalimani ukizingatia kwamba mkalimani hana muda wa kutosha kama walio nao watafsiri.

### 2.1.5 Utamaduni na Mazingira katika Ukalimani.

Newmark (1988)anasema kwamba utamaduni ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha moja mahsusi kama njia yake ya mawasiliano. Msamiati wa lugha kwa kiwango kikubwa hujenga maana za maneno kutokana na utamaduni wa jamii inamozungumziwa lugha hiyo.

Tafsiri kwa hiyo sio tu mchakato wa kiisimu bali pia ni mchakato unaojumuisha maswala yanayohusu utamaduni. Tofauti za kitamaduni husababisha utata katika harakati za kuhawilisha maana kutoka lugha moja hadi nyingine.

Ili kufasiri dhana za kitamaduni mkalimani anawajibika kuelewa tamaduni za lugha zote mbili anazoshughulikia. Ukosefu wa uelewa huu unaweza kusababisha matatizo katika ujumbe katika lugha lengwa .

Nida (1964) Alibainisha kwamba matatizo mengi yanayaoikumba tafsiri ni matatizo ya kitamaduni na kimazingira. Alisema kwamba matatizo hayo husababisha ugumu wa kuweza kupata ufananisho wa maneno kutoka lugha moja hadi nyingine. Kulingana na Nida, majaribio yoyote ya kutatua hayo matatizo yatafaulu tu iwapo mfasiri au mkalimani atazingatia vipengele vinne vya utamaduni navyo ni:-utamaduni wa jamii,utamaduni wa vifaa, utamaduni wa dini na utamaduni wa lugha. Kwa mujibu wa maoni ya Nida mazingira au ekolojia ni sehemu ya utamaduni.

Kila moja ya vipengele hivi hutofautiana katika lugha zozote mbili. Katika Ekolojia kwa mfano Waingereza wana misimu tofauti ya hali ya anga kama vile *winter, summer, Autumn,* na *spring.* Waluo wana misimu miwili tu *Chwiri na Opon* yaani mvua ya masika na ya vuli. Kiangazi huitwa *oro* ilhali baridi ambayo hutokea kati ya mwezi wa saba na nane huitwa *yugni,* hata hivyo *oro* na *yugni* si visawe vya *summer* na *winter.* Ni muhimu kwa mkalimani kufahamu mambo hayo ili kufanikisha mawasiliano kati ya hadhira na mnenaji. Katika ukalimani itambidi atoe maelezo ikiwa visawe havipatikani katika lugha lengwa. Katika uchunguzi wetu kulikuwa na haja ya kuwahoji wakalimani ili kujua kama walifanya juhudi zozote kuelewa utamaduni wa

yule mhubiri ambaye walikalimani ujumbe wake.Jambo hilo lilikuwa muhimu kwa sababu welewa wa utamaduni wa yule anayekalimaniwa ungemfanya mkalimani kufanya kazi nzuri zaidi.

Nida (2002) anasisitiza kwamba lugha ni sehemu ya utamaduni. Ni vigumu kujua mnenaji alinuia kusema nini ikiwa hatuelewi utamaduni wa lugha anayotumia. Kuna baadhi ya nahau ambazo hufungwa katika muktadha asilia ilhali nyingine huweza kutumika katika tamaduni mbali mbali – kwa mfano mtazamo wa Kiafrika juu ya mbuzi na kondoo ni tofauti na ule wa Wayaudi. Wayahudi huthamini kondoo zaidi na kumchukulia mbuzi kuwa ni mnyama mkaidi na kumtumia kutolea mfano ubaya huku kondoo akitumiwa kuonyesha uzuri na unyenyekevu. Katika baadhi ya jamii za Kiafrika kondoo ni kielelezo cha ujinga. Kwa mfano miongoni mwa Waluo, mtu akitaka kulipa mahari kondoo hapelekwi kamwe kwa sababu wanaamini kuwa inaonyesha madharau kwa msichana anayeposwa. Ni ishara kuwa ni mjinga kama kondoo.

Mkalimani katika mkutano wa kidini atakuwa wa manufaa makubwa zaidi kwa hadhira yake iwapo anaweza kutoa maelezo kama hayo. Hatusemi kwamaba kila mara kondoo anapotokea badala yake mkalimani aweke mbuzi.Kile tunachosema ni kwamba mkalimani anaweza kutoa maelezo ya haraka kuwa huko anakozungumzia kondoo alichukuliwa kuwa ni bora zaidi kuliko mbuzi.

### 2.1.6 Mkalimani na Mwegemeo wa Mkalimani

Cremona na Mallia (2001) wanasisitiza kuwa mkalimani lazima atafute habari muhimu kabla ya kuanza kazi yake. Anawajibika kufahamu mambo yote yanayoendelea katika nyanja mbalimbali ulimwenguni kama siasa, maswala ya kijamii na kitamaduni. Habari hizi hupatikana katika magazeti, majarida, redio, na runinga. Maoni hayo ni muhimu katika utafiti huu na tunasisitiza kwamba mkalimani mzuri ni yule ambaye anasikiza vipindi vya redio vinavyotangaza katika lugha anazokalimania ili kupata msamiati mpya na kuimarisha uwezo wake wa kutumia lugha hizo. Katika utafiti huu kwa mfano mkalimani angefaidika mno kwa kusikiza vipindi vya KBC, redio Ramogi ambavyo hutangaza katika lugha ya Kiluo.

Jambo hili ni muhimu kwa wakalimani wa kidini kwa sababu wahubiri hutumia mifano na maelezo kadhaa kutoka nyanja mbalimbali ili kufanikisha ujumbe wanaonuia kupitisha. Jambo hili lilibainika wakati tulipokuwa tukichunguza kalimani.

Kinachobainika hapa ni kwamba mkalimani bora ni yule ambaye ana weledi wa kutosha wa yale yanayoendelea katika ulimwengu unaomzunguka na hata kule anakotoka yule ambaye ujumbe wake unakalimaniwa. Ikiwa mhubiri anatoka Marekani kwa mfano, huenda mhubiri huyo akatumia mifano na maelezo kutoka kwao kutoa ufafanuzi wa ujumbe wake. Mkalimani ambaye hana habari zozote kuhusu nchi ya Marekani hatakuwa wa manufaa makubwa kwa hadhira inayomsikiza. Huenda akawa na matatizo katika kukalimani ujumbe. Lazima ajitayarishe kimbele kwa kusoma magazeti, majarida, kusikiza redio, kujifahamisha na Historia na Jiografia ya kule anakotoka mhubiri. Pia kuna haja ya mkalimani kuzungumza na mhubiri kabla ya mkutano ili ajue lahaja yake na jinsi anavyotamka maneno. Pamoja na hayo kuna haja ya kufahamishana mada itakayozunmziwa.

Peterson (2005) anasema kwamba katika ukalimani kunaonekana mwegemeo kwa kutegemea mkalimani. Kuna miegemeo miwili, mwegemeo wa lugha chanzi na mwegemeo wa lugha pokezi au lugha lengwa. Ukalimani unaoegemea lugha chanzi huonyesha ukuruba zaidi na lugha chanzi katika mambo mengi ikiwemo sintaksia na hata jinsi msamiati ulivyokalimaniwa. Mara nyingi huwa ni moja kwa moja. Ukalimani unaoegemea lugha lengwa kwa upande mwingine huzingatia zaidi wapokezi wa ujumbe, ukalimani huo huonyesha ukuruba na lugha lengwa katika sintaksia yake ambayo huwa imefanyiwa marekebisho ili kuweza kuwiana na ile ya lugha lengwa.

Katika utafiti huu, jambo hili ni muhimu hivi kwamba mwegemeo wa mkalimani huchangia katika kufanikisha au kutinga mawasiliano kati ya hadhira na mhubiri-hususan katika lugha ambazo ni tofauti kimuundo kama vile Kiingereza na Kiluo au Kiswahili na Kiluo. Iwapo mwegemeo wa mkalimani haufanikishi mawasiliano basi hilo linakuwa tatizo katika ukalimani. Peterson pia anasema kwamba nafsi katika ukalimani hutekeleza jukumu muhimu sana katika kuufanya ujumbe kueleweka vyema. Ujumbe hueleweka vyema zaidi kama mkalimani anatumia usemi halisi kwa kutumia nafsi ya kwanza 'ni' kama vile ni yeye ndiye anayesema maneno yale. Hata hivyo wakalimani wengine hupenda kutumia usemi taarifa. Kimsingi usemi taarifa una manufaa yake kama vile mkalimani kutoonekana kuwajibika iwapo anayekalimaniwa amesema jambo lisilopendeza au linaloaibisha. Hata hivyo katika ukalimani wa aina hii muda ni muhimu sana na kwa vile usemi wa taarifa humlazimisha mkalimani kuongeza viunganishi na maneno mengine,jambo hili linaweza kusababisha kukatizwa kwa mkalimani mara kwa mara na kuufanya ujumbe usieleweke. Jambo hilo ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu katika

uchunguzi wetu swala la mkalimani kukatizwa kabla hajakamilisha maneno ya mhubiri linachukuliwa kuwa ni mojawapo ya mambo yanayosababisha matatizo katika ukalimani.

Baadhi ya wakalimani hujaribu kurekebisha maneno ambayo mnenaji ametumia. Wakalimani kama hawa hufikiria kuwa wana jukumu la kufanya hivyo ili kumsaidia anayekalimaniwa. Jambo hilo hata hivyo linaweza kuzua matatizo zaidi. Wakalimani kama hawa hufikiria kuwa wana jukumu la kumuelekeza mnenaji ili kumsaidia. Jambo hilo hata hivyo linaweza kuzua matatizo zaidi. Iwapo mnenaji amesema jambo lisilofaa, basi ni juu yake kuomba msamaha lakini mkalimani apaswa kuwa mwaminifu kwa kazi yake.Jambo hili linaweza kueleweka kwa kutumia mfano ufuatao:

Katika Biblia kuna kifungu katika Zaburi 53:1 kinachosema kuwa ' wajinga husema kuwa Mungu hayupo' Iwapo mhubiri amekuja kuhubiri na kuanza kukariri kifungu hicho kwa kusema "Mungu hayupo" kisha akatulia kidogo na baadaye kuongeza "hivyo ndivyo wajinga husema". Mkalimani ambaye alijaribu kurekebisha maneno ya kwanza ya mhubiri kwa kufikiria kwamba mhubiri alikuwa anakufuru bila ya kukusudia huenda akajikuta matatani kama alikuwa amesema 'Mungu yupo' badala ya kuyasema maneno ya mhubiri vile alivyoyasema. Ili kurekebisha maneno hayo ingembidi aanze upya baada ya kuyasikia maneno yanayofuata.
Jambo hili hutokea kila mara katika ukalimani na ni mojawapo ya mambo tunayotazamia kuchunguza katika utafiti huu.

## 2.2 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya tafsiri ya Nida(1964). Nadharia hiyo ina mambo matatu ambayo ni muhimu kwa utafiti huu.

1. Tafsiri inapaswa kuchukuliwa kama taaluma ya kisayansi.
2. Lugha ni zao la utamaduni na kwamba matatizo yote yanayokumba tafsiri yana msingi wake katika mazingira na tamaduni za lugha hizo mbili.
3. Mtu yeyote anayetaka kufanya kazi ya tafsiri lazima awe na sifa fulani.

Tutazungumzia vipengele hivi kimoja baada ya kingine na kuonyesha vile vipengele hivi vina umuhimu katika utafiti. Kuchukulia tafsiri kama taaluma ya kisayansi ina maana kwamba tafsiri lazima ifuate utaratibu maalum. Katika utaratibu huo kuna haja ya kutambua tatizo, kujitokeza na malengo, kuorodhesha au kujitokeza na mbinu za kufanyia uchunguzi ili kutatua tatizo hilo, kufanya uchunguzi wenyewe na kujitokeza na ripoti ya uchunguzi huo. Katika tafsiri

pia,kuna tatizo ambalo ni ukosefu wa maelewano kati ya watu ambao wanazungumza lugha tofauti na ambao wana nia ya kuelewana. Kulingana na nadharia hiyo lazima kuwe na mbinu za kufanya tafsiri ili kuwawezesha watu hao kuwasiliana.Baada ya tafsiri hiyo kufanywa kuna haja ya kuitathmini ili kuona kama matokeo yake yameafikiana na lengo la kufanya tafsiri hiyo.

Katika ukalimani utaratibu unapaswa kuwa huohuo moja.Katika utafiti huu mkalimani anatarajiwa kuelewa kuwa kuna makundi mawili katika hadhira ambayo hayaelewani na kwamba ni kazi yake kuyafanya makundi hayo kuweza kuelewana. Baada ya kufanya ukalimani wenyewe mkalimani anapaswa kutathmini kazi aliyofanya kwa kuuliza hadhira kama walifaidika kutokana na ukalimani huo. Hii ndiyo sababu utafiti huu utachukulia maoni ya hadhira kuwa ni muhimu katika kujua walivyopokea ujumbe uliokalimaniwa.Maoni hayo yatachukuliwa kama tathmini ya ubora wa ukalimani.

Nida pia alieleza kuwa lugha lazima ijikite katika utamaduni. Hali hiyo huzua swala la mawasiliano kati ya watu wasiotumia lugha moja na ambao hutoka katika mazingira na tamaduni tofauti.

Kuna matatizo mengi yanayozuka tunaposhirikisha tamaduni mbili katika tafsiri au ukalimani.Baadhi ya matatizo hayo ni kama vile:-

- Kutafsiri kijuujuu
- Kuyaepa baadhi ya maneno
- Kutopata uwiano halisi kwa sababu ya tofauti za kimazingira, utamaduni wa vifaa,wa kijamii,wa kidini na wa lugha.

Utafiti huu ulichunguza matatizo katika ujumbe katika kalimani. Kama alivyosema Nida matatizo haya huenda yanatokea kwa sababu ya tofauti za kitamaduni na kimazingira kati ya lugha zinazokalimaniwa mathalani Kiluo-Kiingereza na Kiluo-Kiswahili.

Lugha ya Kiingereza inatofautiana na lugha ya Kiluo kimazingira, kijamii, kidini na katika muundo wake.Lugha ya Kiswahili pia inatofautiana na Kiluo kwa misingi hiyo hiyo. Nida anasema kwamba tofauti za kimazingira huleta matatizo katika kuyapata maneno yanayofanana au yanayowasilisha dhana moja, kwa mfano misimu katika Kiluo na Kiingereza ni tofauti.Waingereza wana *Summer, Autmn, Winter* na *Spring*. Waluo wana *chwiri* na *Opon* yaani mvua ya masika na vuli. Kwa sababu ya tofauti hizi, anayekalimani katika lugha ya Kiluo kutoka Kiingereza anaweza kuwa na matatizo ya kupata visawe anavyovitafuta.

Miundo ya lugha tofauti pia huweza kuleta matatizo. Ili kufanikisha mawasiliano mtu anayetafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine wakati mwingine hulazimika kutumia kirai katika lugha lengwa kuwasilisha dhana ambayo katika lugha chanzi ni neno moja tu. Kwa mfano katika Kiingereza *Dry cow* ikitafsiriwa moja kwa moja katika Kiswahili "Ng'ombe aliyekauka" huleta maana tofauti kabisa.Wao Waingereza wakimaanisha "Ng'ombe aliyeacha kutoa maziwa". Dhana hiyo inaweza kueleweka katika Kiswahili lakini kwa kutumia maneno mengi.

Katika ukalimani, ikiwa mhubiri ametumia neno moja, huenda akafikiria kuwa neno hilo linakalimanika moja kwa moja na kifasiri katika lugha lengwa. Hali hii inaweza kumfanya kuendelea kuongea bila kuelewa kwamba maneno machache aliyotumia yanahitaji maelezo marefu katika lugha lengwa. Jambo hili linaweza kuleta matatizo kwani mkalimani hatakuwa na muda wa kutosha wa kueleza yaliyosemwa na mhubiri. Kukatishwa kalima huku kunaweza kusababisha matatizo katika ujumbe kwenye lugha lengwa. Misingi hiyo ilyoorodheshwa na Nida itatusaidia katika kuweka vigezo vya kutumia wakati wa kuchanganua deta yetu ili kuainisha matatizo yanayojitokeza pamoja na umaratokezi wake katika deta hiyo. Utamaduni wa lugha kama inavyoelezwa na Nida itatusaidia kuchanganua lugha ilyotumiwa katika mahubiri na ukalimani wake katika viwango vya leksia na sintaksia.

Nida pia alizungumzia sifa ambazo zinamfaa mfasiri. Sifa hizo zinamfaa mkalimani vile vile.Nazo ni kwamba:-

- Ajue lugha zote mbili kama lugha yake ya kwanza.
- Azijue tamaduni zote mbili za lugha zinazohusika.
- Ajue mazingira yanayohusiana na lugha hizo mbili.
- Ajue Isimu Nadharia ya lugha zote mbili.
- Ajue aina za tafsiri.

Sifa hizi zilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu mbali na kuangalia matatizo ya kiisimu katika kalimani, tulichunguza wakalimani ili kujaribu kubainisha kama kulikuwa na uhusiano kati ya uwezo wao na mafunzo waliyopata. Kinadharia, mkalimani ambaye amepata mafunzo kuhusu kazi hiyo ana uwezo wa kukalimani vyema zaidi ya yule ambaye hana mafunzo yoyote. Baadhi ya mambo ambayo Nida ametaja hapo juu kama Isimu Nadharia na aina za tafsiri yanaweza kupatikana tu miongoni mwa watu ambao wamepata mafunzo kuhusu kazi hiyo.

## SURA YA TATU
## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa maelezo kuhusu ni mbinu gani tuliyotumia katika uteuzi wa sampuli,ukusanyaji wa deta na namna tulivychanganua deta tuliyopata.

### 3.2 Mpangilio wa Utafiti

Maandishi tuliyopitia yanayozungumzia aina hii ya utafiti yanakubaliana kwa kauli moja kwamba uchunguzi shiriki unafaa zaidi katika kukusanya deta ya aina hii. Aidha kulikuwa na uwezekano wa kutumia kanda ambazo zimenaswa tayari lakini upungufu wake ni kwamba baadhi ya kanda kama hizo zilikuwa zimehaririwa hasa sehemu ambazo mkalimani alikuwa na matatizo. Kanda kama hizo hazingeweza kutupatia deta iliyofaa katika uchunguzi wetu. Mbinu ya kwanza kwa hiyo ilikuwa bora zaidi. Utafiti huu ulifanyika nyanjani. Mtafiti alitumia uchunguzi shiriki, hojaji pamoja na mahojiano.

Tulifikia uamuzi wa kuchunguza mikutano sita ya hadhara ambayo iliandaliwa katika kituo cha mabasi mjini Bondo. Kulikuwa na uwezekano wa kufanya uchunguzi huu katika makanisa mbalimbali lakini hili halikuwezekana. Sababu ni kwamba katika makanisa ibada za Jumapili katika eneo hili huendeshwa katika lugha moja. Wao huweza kuwa na ibada ya Kiluo na kisha ya Kiswahili na kwa hiyo hawatumii ukalimani isipokuwa kanisa moja.Ni katika mikutano ya hadhara ndiyo wao hutumia ukalimani.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Tulihudhuria mikutano ya hadhara ya kidini ambayo lugha ya Kiingereza –Kiluo na Kiluo-Kiswahili zilitumiwa na kunasa mahubiri hayo na kalimani zao kutumia kinasa sauti.
Shughuli za kunaza sauti zilifanywa katika mikutano sita tofauti mjini Bondo. Mikutanao yote iliandaiwa katika kituo cha basi mjini humo. Mitatu kati ya mikutano hiyo ilikuwa ile ambayo mhubiri alitumia lugha ya Kiingereza huku mkalimani akihawilisha maana katika lugha ya Kiluo. Mitatu iliyosalia ilikuwa ile ambayo mhubiri alitumia lugha ya Kiluo huku mkalimani akihihawilisha katika lugha ya Kiswahili.

Katika mikutano yote sita, wahubiri walikuwa watu tofauti na hali kadhalika wakalimani pia walikuwa watu tofauti. Huu uamuzi ulifikiwa ili kuepuka hali ambayo matatizo ya mkalimani

binafsi yangeweza kutia doa uchunguzi huu iwapo angehudumu katika mikutano ya wanenaji tofauti. Matatizo ya mkalimani mmoja hayangeweza kutumiwa kufikia maamuzi yanayohusiana na mambo tuliyokuwa tukichunguza.

### 3.4 Vifaa vya Ukusanyaji Deta

Deta ilikusanywa kwa kutumia kinasa sauti,hojaji ya maoni ya hadhira kuhusu ukalimani na jedwali lililotumiwa kurekodi majibu ya maswali yaliyoongoza mahojiano na wakalimani.

### 3.5 Ukusanyaji wa Deta

Baada ya kunasa sauti, Kanda zilipewa nambari 1-6. Yaliyomo katika kanda hizi yalinukuliwa kwa mwambatano ili kutupa kazi rahisi ya kutuwezesha kulinganisha maneno ya mhubiri na ukalimani wake katika lugha lengwa. Mahubiri na ukalimani wake yaliwasilishwa katika tunukuzi kiambatisho A. Kiambatisho B kilitumiwa kukusanya maoni ya baadhi ya watu waliohudhuria mikutano hiyo kuhusu maoni yao juu ya ukalimani.Nambari ya kila kanda iliandikwa kwenye nafasi iliyoachwa katika kiambatishoA. Lugha ambayo mhubiri alitumia na lugha ya ukalimani iliandikwa kwenye kila tunukuzi.

Baada ya mahubiri kukamilika, mkalimani alihojiwa kutumia maswali yaliyoorodheshwa kwenye Kiambatisho C.Majibu ya mahojiano hayo yaliandikwa kwenye jedwali 2 ukurasa wa 22. Tunukuzi ilifanywa bila kubadilisha neno lolote. Pia baadhi ya watu waliohudhuria mikutano hiyo walipewa hojaji ili kujua maoni yao kuhusu ukalimani katika mikutano hiyo. Maswali hayo yalikuwa maswali funge ambayo majibu yake yalitumiwa kuthibitisha iwapo wao pia waliona kuwa kuna matatizo katika ukalimani wa ujumbe wa mahubiri.Watu hawa walikuwa wale wanaoelewa lugha zote mbili.Watano walipewa hojaji katika kila mkutano.Umaratokezi wa majibu yao ulirekodiwa katika jedwali 1 ukurasa wa 20.

Baada ya mkutano watu wengine ambao hawakuhudhuria mikutano hiyo walipewa tunukuzi za ukalimani ili waweze kuzisoma na kutupa maoni yao kuhusu kueleweka kwake. Baadaye walipewa tunukuzi katika lugha chanzi ili wasome na kutupa maoni yao kama inaeleweka ama la. Tunukuzi zilizotokana na kanda hizo zilipewa nambari ili kuzigawanya katika sehemu mbalimbali kutuwezesha kupata sehemu hizo kwa urahisi. K1-2 kwa mfano ina maana ya kanda ya pili sehemu ya pili. Ikiwa kuna vipande viwili vilivyodondolewa katika

sehemu moja,kipande cha kwanza kimepewa nambari (i) na kile kinachofuata kimepewa nambari (ii) ili kutofautisha dondoo hizo.

Nambari hizi zilitumiwa kuonyesha sehemu ambazo ziliathirika katika uchanganuzi wetu. Ili kuonyesha sehemu hasa inayozungumziwa sehemu mahsusi zimepigwa mstari.

### 3.6 Uchanganuzi wa Deta .

Tunukuzi zote sita zilichanganuliwa ili kubainisha sehemu katika ukalimani ambayo ilionekana kwamba mkalimani alikuwa na matatizo. Maelezo yaliandikwa kuhusu sehemu ambazo zilifikiriwa kwamba ukalimani haukufanyika vyema. Maelezo pia yalitolewa iwapo matatizo hayo au tofauti hizo zingeweza kusababisha kuwa na matatizo kwa ujumbe wa lugha lengwa. Ili kutoonyesha mwegemeo, watafiti walifanya marejeleo pamoja na kutafuta ushauri kutoka kwa wajuzi wengine wa lugha hizo. Katika uchanganuzi wetu tuligundua kwamba tungeweza kufanya kosa kwa kutoa ufasiri ambao haukudhamiriwa na mhubiri au kumkosoa mkalimani kimakosa. Ili kuwa na uhakika kuwa maoni yetu kuhusu kufasiriwa kwa kifungu fulani ni sawa tuliwauliza watu wawili zaidi ili kuthibitisha. Katika sehemu ambazo watu hao hawakukubaliana nasi, tulichukulia kwamba maoni yetu hayakuwa sawa.

Baada ya kasoro hizo kuainishwa umaratokezi wa kila aina ulihesabiwa na kunakiliwa kwenye jedwali 3 ili kubainisha ni kasoro aina gani iliyojitokeza mara nyingi zaidi. Matokeo ya mahojiano na wakalimani yalitumiwa kutathmini ni kwa kiwango gani wakalimani waliweza kujiandaa kabla ya kuanza kufanya kazi yao, pamoja na tajriba na mafunzo yoyote waliyopata kuhusu ukalimani. Matayarisho, tajriba na mafunzo ya kila mkalimani yalinuiwa kutumiwa kama kigezo cha kuamua iwapo mambo hayo yalikuwa na athari yoyote katika utendaji kazi wa mkalimani.

### 3.7 Matatizo yaliyokumba utafiti.

Tulikumbana na matatizo matatu makuu katika utafiti huu.

(i) Mahali ambapo sauti ilinaswa ilikuwa nje karibu na kituo cha magari. Katika eneo hilo kulikuwa na kelele nyingi za mgari, upepo na hivyo mahubiri na kalimani zilizonaswa zilikuwa na kelele nyingi na kufanya kazi ya kupata sauti ya mhubiri kuwa ngumu sana. Hakukuwa na njia yoyote ambayo tungeweza kutumia kukabiliana na hali hii. Hatungeweza kuwaambia waandalizi kuhamisha mikutano hiyo hadi katika majumba ya makanisa yao. Nia yao ya

kuiandaa mikutano hiyo nje ilikuwa ni kuwapata hata wapita njia kusikiza ujumbe waliyokuwa nayo.

(ii) Baada ya kunasa sauti kwenye kanda, changamoto iliyotukumba, ilikuwa ile ya kuandika tunukuzi. Ilituchukuwa muda mrefu sana kwani ilitubidi tusikilize kanda hizo mara kadhaa, wakati mwingine hata zaidi ya mara nne. Jambo hili lilitufanya kuchukua muda mrefu zaidi ya tulivyofikiria utafiti huu ungechukua.

(iii) Katika mikutano ambayo tulihudhuria, watu wengi hawakufurahia kuhojiwa kuhusu jinsi walivyopokea ujumbe. Tunadhani hili lilitokea kwa sababu si jambo la kawaida kwa watu waliohudhuria mikutano kama hii kupatiwa hojaji baada ya mkutano. Ili kuweza kukabiliana na hali hii ilitubidi tuwatumie watu ambao tulikuwa tunawafahamu . Tulifanya hivyo kwa sababu watu hao hawangeweza kutushuku kuwa tulikuwa na nia yoyote mbaya kwa kuwahoji. Kwa upande wa wakalimani, wao hawakuwa na tatizo lolote kutupatia majibu ya maswali tuliyokuwa tukiwauliza.Walishirikiana na sisi vilivyo.

## SURA YA NNE

## UWASILISHAJI WA DETA NA UCHANGANUZI WA DETA

### 4.1. Utangulizi.

Katika sura hii tunatoa matokeo ya utafiti wetu kwa kuwasilisha matokeo ya mahojiano kati yetu na hadhira pamoja na wakalimani. Hatimaye tumeangazia matatizo yaliyojitokeza katika ukalimani tukizingatia vipengele vya sintaksia, leksia, utamaduni wa kijamii, mazingira na vipengele vingine anuwai ambavyo haviwezi kuwekwa moja kwa moja katika vipengele hivyo tulivyotaja.. Katika sehemu hiyo ya matatizo yaliyojitokeza katika ukalimani, tumetumia dondoo ya sehemu zilizoathirika ili kumwezesha msomaji anayeelewa lugha zote mbili kuona jinsi matatizo yalivyotokea.

### 4.2. Maoni ya Hadhira.

Tuliwahoji watu watano katika kila mkutano baada ya mahubiri. Tulitaka kujua kama kwa maoni yao ukalimani huo ulikuwa mzuri. Baada ya kuwahoji watu watano waliohudhuria mikutano yote sita, matokeo yaliyojumlishwa yalirekodiwa katika jedwali 1

**Maoni ya hadhira kuhusu ukalimani.**

| SWALI | JIBU | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | NDIYO | ASILIMIA | HAPANA | ASILIMIA | JUMLA |
| Mkalimani alifanya kazi yake vizuri sana | 10 | 33.3% | 20 | 66.7% | 100% |
| Mhubiri alimpa Mkalimani nafasi ya kutosha | 5 | 16.7% | 25 | 83.3% | 100% |
| Ukalimani ule ungeweza kuboreshwa | 28 | 93.3% | 2 | 6.7% | 100% |

Jedwali la 1

Tulichukulia matokeo ya mahojiano hayo kuwa ni kiashiria cha matatizo katika ujumbe kwenye ukalimani. Kwa mujibu wa matokeo hayo asilimia 33 % walisema kwamba mkalimani alifanya kazi yake vizuri sana. Asilimia 67 % hawakukubaliana nao.

Hii inaonyesha kwamba watu wengi waliohudhuria mikutano hiyo waliamini kwamba ujumbe haukukalimaniwa vizuri. Kwa maoni yetu, ikiwa asilimia hiyo inaamini kwamba ukalimani haukuwa mzuri, basi lazima kulikuwa na matatizo. Inafaa ifahamike hapa kwamba baadhi ya watu waliosema kuwa mkalimani alifanya kazi nzuri walipoulizwa kama ukalimani huo ungeweza kuboreshwa walisema ndiyo. Hiyo inaonyesha kuwa kauli waliyotoa walipoulizwa swali la kwanza haikuwa yenye uhakika.Kama waliamini kuwa ukalimani ulikuwa mzuri hakukuwa na haja ya wao kusema kuwa ungeboreshwa.

Asilimia 16.7 %. pekee ndiyo walisema kuwa mhubiri alimpa mkalimani nafasi ya kutosha. Nafasi tunayozungumzia hapa ni ule wakati kati ya kukamilika kwa maneno ya mkalimani na kuanzishwa kwa maneno ya mhubiri. Wahubiri wakati mwingine walianza kuongea kabla ya mkalimani kukamilisha, maneno yake ya awali. Hii ilimaanisha kuwa mkalimani alilazimika kufanya kazi mbili: - kumsikiza mhubiri huku akiendelea kukalimani maneno yake ya awali. Asilimia 83.3 % walisema kuwa muda huo haukutosha. Hii ina maana kwamba waliona jambo hilo kama kisababishi cha matatizo ambayo mkalimani alikumbana nayo wakati alipokuwa akikalimani. Asilimia 93.3 % walisema kwamba ukalimani ungeweza kuboreshwa . Wanaposema hivyo, hicho ni kiashiria kwamba ukalimani wenyewe haukuwa bora.

Wale watu waliohojiwa walikuwa ni watu ambao wanaelewa lugha zote mbili zilizokuwa zikitumiwa,yaani Kiluo-Kiswahili na Kiingereza-Kiluo. Tuliwahoji hawa kwa sababu hatungeweza kumhoji mtu anayeelewa lugha ya ukalimani pekee. Hangeweza kujua kama yale ambayo mkalimani amesema ndiyo yale yaliyokuwemo katika maneno ya mhubiri au la.

Tulitaka kujua zaidi kama ujumbe wa mhubiri katika lugha chanzi ulieleweka na vile vile kama ukalimani wake unaeleweka. Ili kujua hayo tulichukua tunukuzi hizo na kuwapa watu ambao hawakuwepo wakati wa mahubiri. Kwanza tuliwapa ukalimani ili wasome na kutuambia kama wanauelewa. Asilimia 90 % walisema kwamba hawangeweza kuelewa ujumbe huo vizuri. Hiki kilikuwa kiashiria kwamba waliohudhuria na ambao walielewa lugha ya ukalimani peke yake huenda hawakuelewa ujumbe vyema kama ulivyokusudiwa na mhubiri.

Baadaye tuliwapa tunukuzi za ujumbe wa mhubiri. Baada ya kuzisoma, wote yaani asilimia 100 % walisema kwamba ujumbe huo unaeleweka vizuri sana.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

Kwa mujibu wa uchunguzi huo tuliofanya tuliweza kuthibitisha kwamba wakalimani katika mikutano ya kidini ya Kikristo mjini Bondo wana matatizo katika kukalimani ujumbe wa lugha chanzi. Sababu muafaka inayoweza kutolewa kwa tunukuzi ya lugha chanzi kueleweka huku tunukuzi ya ukalimani kutoeleweka ni kwamba ukalimani huo haukufanyika vyema.

### 4.3. Wakalimani

Kwa vile wakalimani wanatekeleza jukumu muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe kutoka kwa mhubiri hadi kwa hadhira hasa wale ambao hawaelewi lugha chanzi, tuliona kwamba kulikuwa na haja ya kuwachunguza wakalimani hawa. Tulitaka kujua tajriba yao katika kazi ya ukalimani, kama wamepata mafunzo yoyote yanayohusiana na kazi hii ya ukalimani, na kama walifanya matayarisho yoyote siku hiyo kabla ya kuanza kazi ya ukalimani.
Katika uchunguzi wa mafunzo na tajriba ya wakalimani tulipata yafuatayo:-

**Mafunzo na tajriba za wakalimani**

| TAJRIBA (MIAKA) | IDADI YA WAKALIMANI | ASILIMIA % | MAFUNZO |
|---|---|---|---|
| 2 | 1 | 16.67% | _ |
| 3 | 3 | 50% | _ |
| 4 | 1 | 16.67% | _ |
| 6 | 1 | 16.67% | _ |
| JUMLA | 6 | 100% | 0 |

Jedwali la 2

Kama inavyoonekana katika jedwali 2, asilimia 17 % walikuwa wamefanya ukalimani kwa muda wa miaka miwili, asilimia 50 % walikuwa wana uzoefu wa muda wa miaka mitatu, asilimia 17 % alikuwa na tajriba ya miaka minne na asilimia 17% walikuwa na tajriba ya miaka sita.

Hatukuchunguza kwa undani zaidi kama tajriba hii ilikuwa na athari ya moja kwa moja katika utendaji kazi wa mkalimani.

Hata hivyo tunaamini kwamba uzoefu wa muda mrefu katika ukalimani humpa mkalimani umahiri zaidi katika kazi hiyo. Hii ni kwa sababu wakalimani hawa hufanya kazi katika mazingira ambayo sajili haibadiliki sana kwani ni ileile ya dini ya Kikristo tu, maneno ni yale yale na kwa hiyo ikiwa wamesikia maneno yayo hayo na kuyatafsiri kwa muda mrefu, huenda tafsiri zao zikawa bora zaidi.

Tulifikiria kwamba tajriba ya wakalimani hawa haikuwa ya kutosha hasa ikizingatiwa kwamba hawafanyi kazi hiyo kila siku kwani mikutano ya kidini mara nyingi ilikuwa ikiandaliwa mara moja au mara mbili kwa wiki na siyo kila mara mikutano hiyo ilipoandaliwa mkalimani alikuwa mtu yuleyule mmoja. Kuna wakati ambapo walibadilishana mmoja akikalimani wiki hii mwingine naye anakalimani wiki inayofuata.

Jambo la pili tulilochunguza miongoni mwa wakalimani ni mafunzo waliyopata kuhusiana na kazi yao ya ukalimani. Asilimia 100 % hawakuwa wamepata mafunzo yoyote. Tulipofanya uchunguzi wa wahubiri, tulipata kwamba wahubiri hao wamepata mafunzo kuhusu kazi yao ya uchungaji ambayo inahusisha mahubiri pia.

Uchunguzi huo ulituonyesha kuwa uchungaji unachukuliwa kuwa na umuhimu zaidi kuliko ukalimani kwa sababu ikiwa wakalimani wanatekeleza wajibu muhimu jinsi hiyo basi maoni yetu ni kwamba makanisa ambayo yalihitaji huduma hiyo yalikuwa na wajibu wa kuwapa wakalimani hawa mafunzo.

Kwa vile hatukupata mkalimani aliyepata mafunzo ili tuweze kumlinganisha na wale ambao hawakupata mafunzo hatuwezi kusema kwa uhakika kwamba mkalimani aliyepata mafunzo hutenda kazi bora zaidi. Hata hivyo tunaamini kwamba kinadharia, mkalimani aliyepata mafunzo angeweza kufanya kazi bora zaidi.

Hii ni kwa sababu katika mafunzo yake angepitia mambo kama vile:- Aina za tafsiri – tafsiri za neno kwa neno, tafsiri za sisisi na tafsiri maana – ili wakati anapokalimani, mambo hayo yamsaidie kuamua ni aina gani ya tafsiri inayofaa zaidi wakati gani.Kwa ujumla angekuwa na zile sifa ambazo Nida anataja kuwa mtafsiri mzuri anapaswa kuwa nazo.

Nida (2002) katika mahojiano na Neff katika jarida la *Christianity Today* anasisitiza jambo hili kwa kusema kuwa tafsiri bora ni ile inayozingatia visawe amilifu. Anaendelea kusema kwamba mfanano wa kirasimu husababisha matatizo katika katika ukalimani. Katika uchanganuzi wa ukalimani wenyewe, yale ambayo Nida anasema hapa yalibainika wazi zaidi katika sehemu ambazo mhubiri alitumia lugha ya kitamathali.

Mafunzo, kwa hiyo, yangempatia mkalimani ujuzi wa nadharia mbali mbali ambazo zingemsaidia kupambana na matatizo mbali mbali wakati anapotafsiri.

Wakalimani wote tuliowachunguza walikosa mafunzo – wote walikuwa ni watu walioanza kazi yao kupitia kwa mafunzo ambayo mtu hupata kwa kuambiwa kukaa karibu na mfanyi kazi mwenzake na kuangalia yale ambayo anafanya. Wakalimani hawa sawa na maelezo hayo walianza kazi ya ukalimani kwa kuwasikiza wakalimani wengine kanisani wakifanya kazi hiyo. Baadaye waliambiwa wajaribu na hivyo basi kuanza kazi. Umuhimu wa mafunzo pia ni kwamba mafunzo yoyote kuhusu ukalimani au tafsiri huanza kwa kufunza matayarisho ambayo mfasiri anapaswa kufanya kabla ya kuanza kazi hiyo pamoja na mchakato wote wa kufanyia ukalimani wenyewe.

Mahojiano na wakalimani yalibainisha kwamba hakuna hata mmoja ambaye alifanya matayarisho ya awali kabla ya kuanza kufanya ukalimani. Upungufu kama huu uliathiri ukalimani kwa kiwango fulani kama tutakavyoeleza hapo baadaye.Mafunzo yangewafanya waone haja ya kufanya matayarisho.

Wakalimani waliochunguzwa pia walihojiwa ili kutaka kujua kama walipata fursa ya kuongea na wahubiri ambao walipaswa kuwakalimania kabla ya mkutano. Asilimia 33 % kati yao ndio walipata fursa hiyo. Wale wengine asilimia 67 % walikutana na mhubiri kwa mara ya kwanza katika jukwaa. Sababu yetu ya kuzingatia swala hilo la kukutana na kuongea na mhubiri ni kwamba kiisimu kila mtu ana lahaja yake ambayo hujulikana kama lahaja ya kimaeneo. Lahaja za kimaeneo huwafanya watu tofauti kuyatamka maneno kwa namna yao maalum inayotofautiana na watu wengine kutoka sehemu zingine.

Watu wanaofahamiana huelewana vizuri zaidi kuliko wale ambao hawafahamiani. Juu ya hayo, kuna watu ambao wana matatizo ya kimatamshi kama vile vigugumizi na vithembe. Mkalimani akifahamu hayo awali huenda yakamsaida katika kukalimani kwa njia bora zaidi.

Wazungumzi wote wa lugha ya Kiswahili hawazungumzi kwa njia sawa. Kwa mfano, wale wanaotoka sehemu zingine za Kenya huongea Kiswahili kwa namna tofauti na wale wanaotoka pwani mwa Kenya. Licha ya kuwa wazungumzaji wote wanatoka Kenya wana tofauti zao za kilafudhi. Wakenya wengine husema /karamu/ badala ya /kalamu/. Kwa mkalimani ambaye hafahamu matamshi ya mhubiri, matamshi kama hayo yanaweza kumfanya kusababisha matatizo katika ujumbe wa ukalimani hasa ikiwa mkalimani hakuzingatia mukatadha wa ukalimani.

Katika utafiti huu, umuhimu wa kuzungumza na mhubiri ili kuyafahamu matamshi yake ulijitokeza katika 50 % ya mikutano.

Baadhi ya wahubiri waliochunguzwa katika utafiti huu walitoka Marekani. Wahubiri hawa waliotoka Marekani hawakupata fursa ya kuzungumuza na wakalimani wao ili waweze kufahamiana. Mahubiri yalipoanza, mkalimani alikuwa na matatizo makubwa sana katika kuelewa yale ambayo mhubiri alikuwa akisema.Katika mfano mmoja mhubiri alikuwa akisema " *I am called Blaine Rogers*" . Mkalimani alishindwa kuelewa kabisa na hangeweza kupata jina hilo kwa sababu ya matamshi ya Blaine. Mmoja kati ya wahubiri hao licha ya kutoka nchini Kenya, alikuwa akiongea Kiingereza kwa lahaja nzito ya eneo la kwao. Lahaja hiyo ilimtatiza mkalimani hivi kwamba hakusikia baadhi ya maneno ambayo mhubiri huyu alikuwa akisema. Katika hali hiyo matatizo yalitokea sana kwa udondoshaji wa maneno na katika sehemu zingine, uchopekaji. Uchopekaji huo ulifanywa ili kuweza kufidia yale ambayo yalimpita mkalimani. Matokeo yake yalikuwa mabaya kama tutakavyoeleza zaidi hapo baadaye.

Asilimia 100 % ya wakalimani walijua kule ambako mhubiri atakayemkalimania anatoka. Tulifungamanisha jambo hili na swala la matayarisho. Tulitarajia kwamba kujua anakotoka mhubiri ni kidokezo ambacho kingemsaidia mkalimani kufanya matayarisho kwa kiasi fulani. Tulitarajia kwamba wangetumia welewa huo kufanya utafiti zaidi ili kujua utamaduni wa wahubiri, mazingira wanakotoka na habari kuhusu asili yao kwa ujumla.Jambo hili lilikuwa muhimu hasa kwa wale wakalimani waliohudumu katika mikutano ya wahubiri kutoka Marekani. Mambo haya ni muhimu kwa sababu mara nyingi wahubiri wanapokuwa jukwaani, hutoa ufafanuzi kwa kutumia mifano kutoka mazingira yao asilia. Iwapo mkalimani anafahamu hayo kumhusu mhubiri, kazi yake inaweza kuwa rahisi zaidi.

Katika utafiti huu kwa mfano, mmoja wa wahubiri alitoka Arizona na kila alipotoa mifano, alizungumzia mambo ya kule Arizona kuhusu usimamizi wa viwanda na pia utunzaji wa miti na mapenzi waliyo nayo juu ya miti na mazingira K2-18 hadi K2-22. Mwingine naye alizungumzia ndoa za kwao na uhamiaji uliotokea karne tatu zilizopita kutoka Bara Uropa hadi kule Marekani tazama K-13 hadi K-14. Mifano kama hiyo huweza kumzuzua mkalimani ambaye hana ufahamu wowote wa tamaduni hizo na mazingira hayo.Uchunguzi wetu ulionyesha kwamba wakalimani hawakufanya uchunguzi wowote wala kujaribu kufahamu mazingira au utamaduni wa kule anakotoka mhubiri.

Kulingana na Nida (1964) kuzijua tamaduni za lugha zote mbili ni muhimu sana katika juhudi zozote za kutafsiri. Maoni hayo ya Nida ni muhimu pia katika ukalimani.

Nadharia ya taathira lugha ambayo ianaelezwa katika Nadharia Tete ya Sapir-Whorf pia ina msingi wake katika maoni haya. Kwa kutalii utamaduni na mazingira ya lugha ngeni, mkalimani hupanua maonolimwengu wake na kwa kufanya hivyo, humpa uwezo wa kumfanya mtu mwingine ambaye haelewi lugha ngeni kuelewa matukio na maelezo katika lugha hiyo kwa kumtolea ufafanuzi zaidi wakati anapotafsiri au kukalimani.. Wakalimani wote tuliowachunguza hawakutoa ufafanuzi wowote kuhusu mazingira mageni ambayo wahubiri walikuwa wakizungumzia.

Jambo la mwisho tulilolichunguza kuhusu wakalimani ni kama walifahamu awali sehemu ya Biblia ambayo mhubiri angesoma wakati wa mahubiri. 100 % ya wakalimani tuliowachunguza walisema hawakufahamu. Ilionekana kwamba sehemu ambayo mhubiri atasoma ilikuwa siri yake ambayo hakupaswa kumweleza mtu yeyote yule hata mkalimani wake. Kwa maoni yetu, jambo hilo liliwakosesha mahatibu nafasi ya kufanikisha mawasiliano katika mikutano.

Kufahamu sehemu hiyo ya Biblia ni muhimu kwa sababu katika Biblia kila sehemu imejikita katika muktadha maalum na mazingira maalum. Kuna mambo yanayohusu ufugaji, ukulima, mazingira ya jangwa , vita, miungu ya jamii zilizotajwa kwenye Biblia na hata vyombo mbalimbali. Iwapo mkalimani amepitia sehemu hiyo ya Biblia katika lugha ambayo anatarajia kukalimania, huenda asiwe na taharuki wakati anapotafuta vifasiri vya dhana hizo.

Uchunguzi tulioufanya ulionyesha kuwa hicho kilikuwa kisababishi cha matatizo katika sehemu zingine; kwa mfano, katika moja ya mikutano, mhubiri alisoma sehemu ya Biblia inayozungumzia mti unaoitwa *'vine'*. Mkalimani alikuwa na matatizo katika kulitafsiri neno hilo. Katika ukalimani wake alitumia maneno matatu tofauti kwenye mkutano huo huo mmoja. Alitumia 'mzabibu', '*olemo*' na pia '*yath*'.

Katika Biblia ya Kiluo watafsiri walitumia neno ' mzabibu' ambalo kwa uhakika ni neno la Kiswahili. Hata hivyo watu ambao walikuwa wakikalimaniwa na ambao husoma Biblia kwa lugha ya Kiluo tayari wanalikubali neno hilo baada ya matumizi ya muda mrefu katika muktadha wa kidini. Hayo maneno mengine ambayo mkalimani alitumia, kwa hiyo, yalisababisha matatizo. ' *Olemo*' ni tunda lolote na pia '*yath*' ni mti wowote wala si mzabibu peke yake.

Kama mkalimani angedurusu sehemu hiyo ya Biblia katika Kiluo kabla ya mkutano, angefahamu maneno yanayokubalika kutumiwa katika muktadha huo.

Mwisho kuna jambo lililojitokeza ambalo hatukulitarajia. Tuligundua kwamba wale wakalimani waliokuwa wakihamisha mahubiri kutoka lugha ya Kiluo hadi katika lugha ya Kiswahili hawakuwa na Biblia za Kiswahili. Hii ina maana kwamba wakati mhubiri alipokuwa akisoma Biblia katika lugha ya Kiluo, mkalimani alikuwa akifanya tafsiri ya hapo kwa hapo. Jambo hili lilisababisha matatizo kwani hawangeweza kutafsiri baadhi ya sehemu sawasawa.
Tafsiri za Biblia katika lugha mbalimbali ni zao la kazi iliyochukua muda mrefu. Jaribio lolote la kufanya tafsiri papo kwa hapo kama ilivyokuwa katika mikutano hiyo si jambo la busara.
Ingekuwa bora zaidi kama wakalimani wangekuwa na Biblia iliyotafsiriwa katika lugha pokezi na kusoma maneno yalivyoandikwa.

Kwa mujibu wa uchunguzi huu kuhusu wakalimani, tunaweza kusema kuwa kwa ujumla, wote walichukulia kazi hiyo kijuujuu bila kuzingatia kwamba kuna matayarisho yoyote ambayo walipaswa kuyafanya ili kuwawezesha kufanikisha kazi yao. Hivyo walichangia kuongeza matatizo katika ujumbe wa lugha chanzi.

### 4.4. Matatizo yaliyojitokeza katika Ukalimani

#### 4.4.1. Utangulizi

Baada ya tunukuzi kufanywa, tulifanya uchanganuzi wa vipengele ili kubainisha ni aina gani za matatizo yaliyojitokeza. Tulizingatia matatizo ya kiisimu katika viwango viwili- yale yaliyohusiana na sintaksia na yale yaiyohusiana na leksia. Ingawa mambo hayo mawili yalionekana kuleta athari katika kiwango cha maana au semantiki, hatukuchukulia tatizo la semantiki kama tatizo linalojisimamia bali linalosababishwa na matatizo hayo mawili. Mbali na hayo kulikuwa na matatizo ya kitamaduni ya kijamii, kimazingira na mengine anuwai ambayo hayawezi kuwekwa moja kwa moja katika matapo hayo tuliyotaja.Matokeo ya uchanganuzi wetu yamewasilishwa katika jedwali 3.

**Aina za matatizo katika ukalimani.**

| AINA YA MATATIZO | KIINGEREZA KILUO Umaratokezi | % | KILUO KISWAHILI Umaratokezi | % | JUMLA % |
|---|---|---|---|---|---|
| KILEKSIA | 27 | 26.47 | 18 | 16.67 | 43.14 |
| KISINTAKSIA | 9 | 8.825 | 9 | 8.825 | 17.65 |
| KITAMADUNI | 1 | 0.98 | 0 | 0 | 0.98 |
| KIMAZINGIRA | 2 | 1.96 | 0 | 0 | 1.96 |
| ANUWAI | 22 | 21.56 | 15 | 14.71 | 36.27 |
| JUMLA | 61 | | 42 | | 100 |

Jedwali 3

Matatizo ya kileksia yalijitokeza mara nyingi zaidi. Matatizo ya kileksia hapa ina maana kwamba mkalimani alitumia neno lisilofaa au kushindwa kupata neno ambalo angeweza kutumia; kwa hiyo, kuliacha neno hilo bila kutafsiriwa au kutumia neno lilo hilo vile lilivyo katika lugha chanzi bila jaribio lolote la utohozi. Kitendo hicho japo kiisimu huweza kuitwa ukopaji, ni kitendo kisichofanikisha mawasiliano hasa ikizingatiwa kwamba wanaokalimaniwa wanasikia neno hilo kwa mara ya kwanza. Si kwamba ukopaji ni mbaya, kwa hakika hii ni njia mojawapo ya kupanua lugha. Hata hivyo maneno yaliyokopwa hupitia mchakato fulani ambapo neno hilo hatimaye hukubalika katika lugha hiyo. Kwa hivyo ukopaji ambao hufanywa na mkalimani ghafla tu ili kuepuka aibu ya kushindwa kutafsiri hadharani husababisha matatizo au huwafaidi tu wale walio na uwezo wa kuelewa lugha zote mbili. Kwa wale ambao hawaelewi lugha zote mbili, mawasiliano yatakuwa yametingwa kama mkalimani alivyofanya katika neno '*visa*'.Jambo hili limefafanuliwa kwa undani katika sehemu inayofuata.

Matatizo ya kileksia yalifuatwa na matatizo ya kisintaksia katika umaratokezi. Haya yalijitokeza kwa mkalimani kuhamisha sintaksia ya lugha chanzi hadi katika lugha lengwa kwa kutafsiri maneno tu bila kupanga upya sarufi ile ili iweze kuwiana na ile ya lugha lengwa.
Jambo hili lilisababisha matatizo katika sehemu mbalimbali kama tutakavyoeleza katika uchanganuzi wa kina wa tatizo hilo.

Aidha, kulikuwa na matatizo anuwai ambayo yalikuwa ni pamoja na kupuuza sehemu zingine, kuongeza maneno ambayo mhubiri hakusema. Kutokamilisha kukalimani sehemu fulani kulisababishwa na mambo mawaili. Sababu ya kwanza ni kukatizwa na mhubiri, na pili ni mkalimani kutosikia yale ambayo mhubiri amesema na kwa hivyo kuacha sehemu zingine bila kutafsiriwa. Mambo haya yote yalichangia katika kusababisha matatizo katika ujumbe wa lugha lengwa.

**4.4.2. Matatizo ya Kileksia.**

Matatizo haya ya kileksia ndiyo yalikuwa mengi zaidi yakilinganishwa na matatizo mengine. Matatizo haya yalitokea kwa njia mbalimbali. Katika baadhi ya sehemu mkalimani alitumia neno ambalo halifai na kuleta utata wa kisemantiki. Katika sehemu zenye utata kama huo hakuna mantiki katika tungo. Kwa mfano katika sehemu moja mkalimani alisema "anaacha kulipa mahari kwa watoto wa shule" katika jaribio la kukalimani kuacha kulipa *skul fis*

Katika baadhi ya sehemu mkalimani aliacha maneno mengine bila kuyatafsiri. Tulichunguza iwapo maneno hayo yaliyopuuzwa yana vifasiri katika lugha lengwa.Kama vifasiri vilipatikana, kauli yetu ilikuwa ni kwamba kupuuzwa huko kulitokana na upungufu wa mkalimani. Ikiwa ilitokea kwamba kifasiri hakikupatikana , kauli yetu ilikuwa ni kwamba jambo hilo lilitokana na tofauti kati ya lugha hizo mbili.

Hali hiyo ya kutoweza kueleza dhana fulani katika lugha nyingine licha ya kuwa dhana hiyo ipo katika lugha chanzi ndiyo ilielezwa katika Nadharia ya Taathira Lugha. Jambo hilo hutokea kwa sababu lugha zozote mbili huwa na maonolimwengu tofauti na kwa hiyo inaweza kuwa vigumu kuhamisha maana kutoka lugha moja hadi nyingine, Sapir na Whorf ambao walifafanua nadharia hiyo zaidi waliona kwamba licha ya tofauti hizo, lugha zozote mbili lazima ziwe na uhusiano fulani japo si kwa kila kiwango. Waliona uhusiano huo kuwa ndio unawezesha lugha moja kutafsiriwa katika lugha nyingine. Maoni hayo yalikuwa na umuhimu katika utafiti huu hivi kwamba sehemu ambazo hazikufasirika zilisababisha matatizo katika lugha lengwa.

Tuliangazia ya sehemu hizo na kuonyesha namna matatizo hayo yalivyotokea. Ni muhimu kusema hapa kwamba kutafsiri neno visivyo huweza kusababisha matatizo na vile vile kutotafsiri neno kwa kulipuuza pia huweza kusababisha matatizo. Tulitumia mifano ifuatayo kuthibitisha hoja zetu: -

K1-3 Mhubiri: *Was I born for this? Was I born for this?*

Mkalimani: *Ne onywola ne gin?*

Katika kifungu hicho kulikuwa na hali ya kutoelewana kati ya mhubiri na mkalimani. Mhubiri alikuwa akiuliza, ' Nilizaliwa kwa ajili ya kazi hii?'
Mkalimani naye akatafsiri 'Nilizaliwa kwa ajili ya hawa?' kilichotokea hapa ni kwamba mhubiri aliposema *this* mkalimani alifikiria alisema *these*. Tofauti hiyo imesababisha matatizo katika yale ambayo mhubiri alikuwa akisema. Huu ni mfano wa jinsi fonolojia inavyoweza kuleta matatizo katika ukalimani.Katika lugha ya Kiluo hakuna sauti /z/.Mara nyingi wazungumzaji wa lugha hii wanapokumbana na sauti hutumia sauti /s/.Jambo hilo lilimfanya mkalimani kukosa kutambua tofauti kati ya neno *this* na *these* kwa hiyo kumfanya kutumia neno lisilofaa katika kukalimani sehemu hiyo.

K1-3 ii Mhubiri: *You don't know the excitements that I experience.*

Mkalimani*: Ok ung'eyo mor ma asiko aneno.*

Maneno ambayo mkalimani alitumia kama vifasiri vya maneno *Excitement* na *Experience* si mwafaka. Kwa neno la kwanza *excitement* alitumia *'Mor'*.Neno mor lina maana ya furaha ya kawaida inayolenga maana sawa na *happiness.* Neno *excitement* si furaha tu bali ni msisimko na kwa hiyo angetumia neno *ilo* badala ya *mor.* Ametumia neno *aneno* kama kifasiri cha neno *experience. Anen* ina maana ya ona. Katika muktadha huo, neno *awinjo* ambalo lina maana ya hisi na sikia lingefaa zaidi. Kinachobainika hapa ni kwamba mkalimani alitumia maneno sahili ambayo hayaelezi kwa ukamilifu ujumbe wa mhubiri.

K1-4Mhubiri*: He was waiting to see my passport and my visa.*

Mkalimani: *Kendo ne orito neno passpost na, gi visa mara bende.*

Katika kifungu hicho, maneno hayo mawili *"passport"* na *"Visa"* hayakukalimaniwa. Hatukutarajia kwamba maneno hayo yapatikane katika lugha ya Kiluo.

Hii ni kwa sababu miongoni mwa waluo hakukuwa na usafiri kati ya nchi ambapo stakabadhi kama hizo zingetumiwa. Hata hivyo kulikuwa na haja ya kutoa maelezo kuhusu stakabadhi hizo. Mkalimani hakutoa maelezo yoyote. Hatari ya kutofanya hivyo ni kwamba kama katika hadhira hiyo kulikuwa na watu ambao hawaelewi Kiingereza hata kidogo, hawangeweza kujua kile ambacho kilikuwa kinazungumziwa.

K1-7 Mhubiri: *The spirit of the Living God.*

Mkalimani*: Roho mar Nyasaye.*

Ingawa inaonekana kwamba mkalimani alitumia neno ambalo si la Kiluo "Roho", neno hilo limekubaliwa katika sajili ya dini kwa sababu katika lugha ya Kiluo, hakuna neno ambalo linaweza kuelezea dhana hiyo ya *Spirit* kwa ukamilifu.

Hata hivyo, mkalimani alipuuza neno *living*. Neno *living* lipo katika lugha ya Kiluo-*ngima* na kwa hiyo hakuna sababu za mkalimani kulipuuza neno hilo. Kupuuzwa kwa neno hilo kulisababisha tatizo la sehemu hiyo kutoeleweka vyema kwa sababu neno hilo kila mara hutumiwa kutofautisha kati ya Mungu na miungu. Mungu aliye hai hubainisha uwezo wa Mungu huyo tofauti na miungu iliyochongwa ama sanamu zinazoabudiwa katika baadhi ya imani za kidini. Angesema *Roho mar Nyasaye mangima* maanake 'roho wa Mungu aliye hai'

K1-10 Mhubiri*: I have a passport to the next world.*

Mkalimani: *Antie gi otiko mar piny machielo.*

Katika usemi huo mkalimani alitumia neno *otiko* kwa maana ya *Passport*. Neno hilo ni utohozi kutoka Kiingereza wa neno *Ticket*. Si sawa kwa mkalimani kutumia neno hilo kwa sababu mbili; kwanza ni kwamba, tayari alikuwa ameshatumia neon *Passport* moja kwa moja katika ukalimani wake hapo awali. Ingekuwa bora zaidi kama angeendelea kulitumia neno hilo vile vile kila mara linapojitokeza. Akibadilisha alivyofanya katika kifungu hicho huenda hadhira ikakanganywa wakifikiria hilo ni neno tofauti.

Pili, dhana ya *Passport* na *Ticket* ni tofauti kabisa. *Ticket* hupewa msafiri baada ya kulipa nauli ya usafiri.

*Passport* ni hati inayompa mtu ruhusa ya kusafiri kutoka nchi moja hadi nchi nyingine. Mkalimani anapotumia neno *Otiko*, dhana inayojitokeza ni kwamba kuna malipo fulani inayotolewa ili watu waweze kufika mbinguni.

Hiyo inaleta tatizo la ujumbe wa mhubiri kueleweka visivyo. Mhubiri alikuwa aking'ang'ana kueleza kwamba hakuna chochote ambacho mtu anapaswa kulipa ili kupata idhini hiyo ya kurithi uzima wa milele.

K1-14 Mhubiri*: It was an experience.*

Mkalimani*: Ne en gima atimo.*

Ukalimani huo *Ne en gima atimo* maana yake ni 'ni kitu nilichofanya'.
Hayo si yale ambayo mhubiri alikuwa akisema. Mhubiri alikuwa akieleza tukio la kukutana na nyanyaye mkewe kuwa lilikuwa la ajabu katika maisha yake. Mkalimani alishindwa kupata kifasiri cha *experience* wala kueleza maana ya neno hilo sawasawa katika muktadha. Ingekuwa bora zaidi kusema '*en gima ne akale'*.Neno *akale* lina maana ya kupitia. Katika muktadha huo neno hilo lingesimamia *experience.*

K1-11 Mhubiri*: I thought it was my fault and I knew that right away.*

Mkalimani: *Ne a paro ni en wachna, ne ang'eyo mana kamano.*

Katika maneno ya mkalimani, maana ya maneno hayo ya mhubiri haijatokea ipasavyo. Anachosema mkalimani hapa ni *Nilifikiria ni neno langu.* Tatizo hapa ni kwamba mkalimani hakutumia kifasiri kifaacho cha neno *fault* ili kuleta maana kwamba alijua nyanyaye mkewe alimfikiria kuwa ndiye mwenye makosa ya kumbadilishia dhehebu mjukuu wake.

Kosa hilo moja la kutumia neno lisilofaa limeifanya sehemu hiyo ya ujumbe ama kutoeleweka kamwe au kueleweka visivyo na kusababisha tatizo la sehemu hiyo kutoeleweka.Angesema *"Ne nenore ni en kethona"* ambayo ina maana ya Ilionekana lilikuwa kosa langu.

K1-20 Mhubiri: *He was going to hang on the cross.*

Mkalimani: *Ne ong'eyo ni odhi dere e bao.*

Katika sehemu hii kuna matatizo mawili. Tatizo la kwanza ni kwamba mkalimani alitumia neno "*Bao*" kama kifasiri cha neno "*Cross*".

Hata hivyo neno hilo *'bao'* si mwafaka kwa sababu kwa muda mrefu makanisa katika maeneo ambayo Kiluo huzungumzwa yamekuwa yakitumia neno la Kiswahili "Musalaba". Hata "*Bao*" limetokana na lugha ya Kiswahili lakini haliwakilishi dhana hiyo ya musalaba sawasawa.

Jambo la pili ambalo ndilo limesababisha matatizo makubwa katika kifungu hicho ni neno "*hang*". Katika ukalimani, mfasiri alitumia neno "*dere*". Neno hilo katika Kiluo lina maana ya "kujitia kitanzi".

Kulingana na mafunzo ya imani ya Kikristo, Yesu hakujitia kitanzi bali alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za walimwengu. Tunaamini mkalimani alisababisha tatizo hapa kwa sababu alikuwa anajaribu katafsiri neno "*Hang*".Katika Kiingereza cha Kimarekani wao hutumia *hang* badala ya "*crucified*". Ukosefu wa welewa huu ulimfanya kutokalimani neno hilo sawasawa na kwa hiyo kusababisha matatizo.

K1-21 Mhubiri: *Jesus meant something special.*

Mkalimani: *Yesu nomino gimoro makende.*

Katika kifungu hicho mkalimani alitumia uhulutishaji wa Kiluo na Kiingereza ili kupata neno "nomino" "ne meant" → ne omino → nomino.

Uhulutishaji huu unawafaa watu ambao wanaelewa lugha zote mbili,Kiingereza na Kiluo. Hata hivyo wale ambao hawaelewi Kiingereza hawawezi kujua mkalimani anamaanisha nini na kwa hiyo kusababisha matatizo. Kama sentensi ya mkalimani haingeanza na neno Yesu, basi huenda tafsiri ingekuwa rahisi. Angesema *wach Yesu no ne nigi tiende makende.*

K1-32 Mhubiri: *It's a character of tenderness, kindness, humility, meekness and longsuffering.*

Mkalimani: *En ranyis mar ng'wono, mohore, bedo ratiro, kendo bedo maonge mibadhi.*

Katika sehemu hii, maneno mengi ambayo yalitumiwa na mhubiri hayakukalimaniwa. Ni maneno *Kindness* na *Humility* pekee ndiyo mkalimani alipata vifasiri vyake sawasawa. Hayo maneno mengine ama yamepuuzwa au kukalimaniwa visivyo.

Neno *Character* lilikalimaniwa kuwa *ranyisi*. Neno hilo la Kiluo *ranyis* lina maana ya mfano na kwa hiyo haliwezi kuwa kifasiri kifaacho cha neno la Kiingereza *character* ambalo tunajua lina maana ya 'tabia' ambalo kifasiri chake katika Kiluo ni *tim.*

Mkalimani vile vile alishindwa kutafsiri neno *tenderness* licha ya kwamba kuna kifasiri chake katika lugha ya Kiluo *muolo* . Tulifikiria kwamba huenda kushindwa huku kulitokana na mkalimani kutosoma Biblia katika lugha ya Kiluo. Hata hivyo neno *Longsuffering* kama inavyotumiwa katika Biblia ni ngumu kutafsiri. Tafsiri ya neno hili katika Kiluo huweza kuleta dhana ya "Kusumbuka kwa muda mrefu" jambo ambalo si ukweli katika muktadha huo. Kile ambacho Biblia inamaanisha hapa ni uvumilivu wa Mungu.Ugumu wa tafsiri wa dhana kama hiyo huonyesha tofauti ya kimaonolimwengu kati ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiluo. Mifano kama hii hufanya ujumbe wa lugha chanzi kutohamishwa vyema katika lugha lengwa.

Kwa kukosa vifasiri mkalimani alitumia maneno ambayo huwa na maana tofauti. Neno *mibadhi* lina maana ya *corruption* – ufisadi, *bedo ratiro* ina maana ya *honest* – mwaminifu. Hii ina maana kwamba wale wanaoelewa lugha ya Kiluo peke yake walipata maana tofauti kabisa katika kalimani hizo.

K1-34 Mhubiri*: Why do I do what I do? Answer Because of Jesus.*

Mkalimani: *En ango momiyo atimo gima atimo? Ang'sa Nikech Yesu.*

Tatizo lililoko katika sehemu hii ni kwamba mkalimani hakukalimani neno *"answer"* bali amelitohoa na kuwa *ang'sa*. Utohozi huo haufai kwa sababu mbili. Kwanza ni kwamba kuna neno la Kiluo *duoko* ambalo lingeweza kutumiwa.

Pili ni kwamba utohozi kama huo hutegemea uwezo wa watu wanaokalimaniwa kuelewa lugha chanzi na kama hawaelewi basi hauwafai chochote isipokuwa kama neno ni la kionomatopia- ambalo linaiga mlio wa kitu fulani.

K2-5 I Mhubiri*: Jesus said, I am the true vine.*

Mkalimani: *Yesu ne owacho ni an e mzabibu.*

Katika ukalimani, neno t*rue* lilipuuzwa. mkalimani alisema tu 'Yesu alisema mimi ndiye mzabibu' badala ya msisitizo wake kwamba 'mimi ndiye mzabibu wa kweli. Japo tofauti haionekani kwamba ni kubwa sana, ujumbe uliokusudiwa hadhira haukuwafikia sawasawa. *True* ina umuhimu mkubwa katika imani ya Kikristo. Angesema *Yesu ne owacho ni an e mzabibu mar adier.*

Katika sehemu hiyohiyo, neno *Vine* lilikalimaniwa kuwa *mzabibu* neno hilo si neno la Kiluo bali ni neno la Kiswahili. Tunashuku, hilo lilifanyika kwa sababu katika eneo hili hakuna mti wa mzabibu. Hata hivyo neno hilo limetumiwa kwa muda mrefu katika eneo hili hivi kwamba watu wanajua kuwa ni aina ya mti. Kwa hiyo matumizi yake hayakusababisha matatizo. Hata hivyo hatudhani kama watu katika eneo hili wamewahi kuona mzabibu. Kwa hiyo kulikuwa na haja ya mkalimani kutoa maelezo.

K2-5 ii Mhubiri: *You are the branches of Jesus.*

Mkalimani*: Un e bede yath.*

Hapa, mkalimani alipuuza neno 'Jesus' na badala yake alitumia neno *Yath* ambalo lina maana ya mti. Mhubiri alitumia neno 'Jesus' kitamathali kwa maana kwamba Yesu ni sawa na mzabibu na waumini ni matawi ya mti huo. Inaonekana mkalimani aliona ugumu kuchukulia Yesu kuwa mti na kwa hiyo akaonelea kuweka neno mti badala ya Yesu. Badiliko hilo limefanya maana kupotea. Sababu ni kwamba ile dhana ya kuwa matawi ya Yesu kitamathali imepotea. Angesema *un e bede Yesu.*

K2-13 Mhubiri*: No matter what wiser, the blood of Jesus flows through us.*

Mkalimani*: Remb Yesu mol kuomwa.*

Mkalimani amepuuza maneno *No matter what wiser* maneno hayo yapo katika lugha ya Kiluo *kata ka iriek nadi.* Mhubiri alikuwa anajaribu kusema kuwa hata ikiwa mtu ni mwerevu

namna gani, damu ya Yesu inatiririka katika mishipa yetu. Huenda mkalimani hakuelewa maneno ya mhubiri vizuri kwa sababu ya namna alivyotumia Kiingereza.

K2-16 Mhubiri: *God who changes situations.*

Mkalimani: *Nyasaye maloko paro.*

Mkalimani hakutumia neno lifaalo kukalimani neno *situations*. Ametumia neno *paro*. Ukalimani huo si sawa kwa sababu neno hilo lina maana ya mawazo au fikira. Mhubiri alikuwa akizungumzia "hali" kwamba ni Mungu ambaye anaweza kubadilisha hali. Mkalimani angesema *Nyasaye makelo lokruok.*

K2-18 Mhubiri*: He prunes the branches.*

Mkalimani*: Odoyo.*

Mkalimani alitumia neno *Odoyo* kutafsiri neno *Prune*. Neno hilo la Kiluo ambalo mkalimani alitumia lina maana ya kupalilia ambalo si sawa na *prune.*Neno ambalo lingefaa zaidi ni *lwero.* Hata hivyo neno hilo pia si mwafaka katika kueleza kitendo hicho. Maana yake ni kukata matawi bila ya kueleza ni kwa sababu gain. *Prune* kwa upande mwingine hufanywa ili mti uweze kustawi na kuzaa matunda mengi zaidi. Ingefaa aseme *lwero mondo onyaa* yaani kukata ili kutoa mazao zaidi.

K2-24 Mhubiri*: I am a person responsible for several factories.*

Mkalimani: *Owadwa ni en jatend factoche.*

Katika ukalimani huo Mkalimani ametohoa neno " factories" *factoche*. Kama tulivyosema hapo awali, utohozi wa aina hii huwafaidi tu wale ambao wana weledi wa lugha zote mbili. Wale ambao hawaelewi Kiingereza hawawezi kuelewa mhubiri alisema nini.

K2-26Mhubiri: *Pressure is too much.*

Mkalimani: *Lweny ger.*

Huu ni mfano wa tatizo ambalo mkalimani ametumia maneno ambayo ni tofauti kabisa na maneno ya mhubiri. Neno *Pressure* hapa lilimaanisha shindikizo kulingana na mhubiri. Mkalimani alitumia *lweny ger* maneno ambayo yana maana ya vita ni vikali. Katika kiluo ingekuwa bora kusema *gik ma odiyi.*

K3-1 Mhubiri*: Rejoice because our saviour is listening.*

Mkalimani: *Bed maili ili nikech intie eiye.*

Mkalimani hakupata kifasiri kafaacho cha neno *rejoice* ambalo maana yake ni kuwa na furaha. Neno alilotumia lina maana ya msisimko ambalo lingefaa kama neno la Kiingereza lililokuwa likitafsiriwa lingekuwa *excited.* Sehemu ya mwisho ya sentensi hiyo imekalimaniwa visivyo. *listening* ni anatusikiza *winjowa* katika Kiluo. Lakini badala ya kutumia neno hilo mkalimani alitumia maneno *intie eiye* ambayo yanamaanisha 'umo ndani'. Haifahamiki ni kwa nini mkalimani alitumia maneno hayo lakini kamwe si kiwakilishi cha neno *listening.*

K3-6 i Mhubiri: *Jesus wants you.*

Mkalimani: *Yesu oor.*

Katika sehemu hii Mkalimani ametumia neno ambalo halifai *wants you* ni anakutaka. Neno ambalo mkalimani ametumia *oor* lina maana ya "ametumwa"; kwa hiyo, badala ya mkalimani kusema "Yesu anakutaka" yeye amesema "Yesu ametumwa".

K3-6 ii Mhubiri: *He wants to save you from the storm.*

Mkalimani: *Odwa ni mondo ogoli e lwet jachien.*

Huu ni mfano wa matatizo ambayo mkalimani hutumia maneno ambayo mhubiri hakusema. Tatizo hilo limetokea katika sehemu ya mwisho ya sentensi hiyo. Neno *storm* ambalo lina maana ya dhoruba limekalimaniwa kuwa *lwet jachien* ambalo maana yake ni "mikono ya shetani" kuna neno la Kiluo ambalo mkalimani angeweza kutumia – *apaka.*

Hata hivyo kwa sababu ambazo hazieleweki, mkalimani alitumia maneno yake mwenyewe ambayo hayawakilishi dhana ambayo mhubiri alitaka kueleza. Mhubiri alikuwa na nia ya kueleza kuwa Yesu anataka kuwaokoa kutokana na maisha ya misukosuko ama taabu. Pengine mkalimani alitumia 'mikono ya shetani' ili kutia chumvi katika maneno ya mhubiri ili kuiwezesha hadhira kuona kuwa kuna hatari inayotakikana waepukane nayo. Kutia chumvi huku hakufai kwa sababu kunasababisha kutoeleweka kwa ujumbe wa mhubiri.

Jaribio kama hilo ni sawa na mkalimani kutoa mahubiri yake mwenyewe. Kama hakuna kifasiri katika lugha lengwa, mkalimani ana uhuru wa kutoa maelezo yake. Lakini maadamu kifasiri kipo, basi hana haki kufanya alivyofanya katika kifungu hicho.

K3-6 iii Mhubiri: *That those of you.*

Mkalimani: *Ji mang'eny.*

Mhubiri alisema *those of you* ambayo ina maana ya "baadhi yenu".
Mkalimani kwa upande wake alitumia *Ji mang'eny* ambayo maana yake ni "watu wengi".
Hili pia ni jaribio la kuchagua maneno ambayo yananuiwa kutia chumvi juu ya yale ambayo mhubiri alisema. "baadhi yenu" si sawa na "watu wengi" na kwa hiyo ujumbe wa mhubiri ulikalimaniwa visivyo. Angesema *jomoko kuomu.*

K5-1 Mhubiri: *Amor ahinya gi jobondo nyaka nyocha abi ka.*

Mkalimani: "Nafurahia na watu wa Bondo hadi nije mahali hapa".

Mhubiri alisema kuwa amefurahishwa sana na watu wa Bondo tangu alipokuja Bondo. Mkalimani alitumia neno "hadi" badala ya "tangu" matumizi hayo ya neno hadi yalizua fahiwa ya watu waliohudhuria kupata dhana kwamba kuja kwake Bondo ni jambo litakalofanyika siku za usoni. Jambo hili lilikuwa na uwezekano wa kuzua utata kwa sababu mhubiri tayari alikuwa Bondo na kwa hiyo neno "hadi" halikufaa kamwe.

K4-4 Mhubiri: *Nyaka yo moluwo kodhi lamo Nyasaye be ok one kaber.*

Mkalimani: "Hata njia anayofuata ili aabudu Mungu haoni wema".

Mfasiri alitumia neno "wema" badala ya neno nzuri. Mhubiri alisema hata njia anayofuata anapoenda ibadani haoni kuwa ni nzuri. Mhubiri alikuwa na maana ya woga ambao mtu anaweza kuwa nao kwamba huenda kuna watu wanaomfuata kwa nia ya kumdhuru.Katika tafsiri ya mkalimani, neno mema alilotumia limefanya sehemu hiyo kueleweka kama kwamba mbinu anayotumia katika ibada haimletei uzuri. Kutokana na neno hilo moja, maana imebadilika na kwa hivyo ujumbe wa mhubiri umepotoshwa.

K4-5 Mhubiri; *Nyamrerwa.*

Mkalimani: "Tabibu wa kisiri".

Neno *nyamrerwa* katika lugha ya Kiluo ina maana ya tabibu. Mkalimani aliposema tabibu wa kisiri dhana inayojitokeza ni ile ya waganga ambao ndio watu huwaendea kisirisiri. Uhusiano kati ya *nyamrerwa* na wateja wake huwa si wa kisiri. *Nyamrerwa* ni neno la Kiluo linalomaanisha daktari au tabibu.

K4-6 Mhubiri: *koro ka chandruok omake.*

Mkalimani: "Wakati shida limemkabidhi".

Tatizo lililoko hapa ni lile la kutumia neno linalokaribiana kimatamshi na neno jingine. "*chandruok omake*" ina maana ya "shida zinapomkabili".Mkalimani kwa hiyo alitumia neno kabidhi badala ya kabili. Tafsiri hiyo ya Kiswahili kwa hivyo haieleweki.

K5-1 Mhubiri *: Nyasaye nigi tiende kwom kelowa ka .*

Mkalimani: "Mungu ako na mguu kwa kutuleta hapa".

Ingawa tulishughulikia sehemu hii katika sehemu ya sintaksia, tumeirejelea kwa sababu mkalimani alitumia neno lisilofaa ambalo ndilo lilileta matatizo ya maana katika ujumbe.
Neno *tiende* linaweza kuwa na maana ya "maana", "mguu" ama "sababu" kwa kutegemea muktadha. Iwapo mkalimani ametafsiri bila kuzingatia muktadha, basi matatizo yanaweza kutokea kama ilivyokuwa katika kifungu hicho. Neno ambalo Mkalimani alifaa kutumia ni 'sababu' na wala si 'mguu'. Kimantiki,Mungu hawezi kuwa na mguu kutuweka mahali fulani,

anaweza tu kuwa na sababu ya kuwaweka watu mahala fulani.Tatizo lililotokea hapa ni lile la uteuzi wa kimantiki.

K5-2 Mhubiri. : *Nyowuoyo kodwa kuom gima iluogo ni yie.*

Mkalimani: "Alituongelesha kuhusu kitu kinachoitwa uzima".

Hapa mkalimani alitumia neno 'uzima' ambalo si tafsiri ya neno *yie.* Neno *yie* maanake ni imani. Imani na uzima si visawe.Kwa hiyo hicho kifasiri hakifai. Huenda tatizo hilo lilitokana na mkalimani kukosa makini na kutosikia kile ambacho mhubiri alisema. Uzima katika Kiluo ni *ngima.* Neno ambalo ni tofauti kimatamshi na neno *yie.* Kwa vile mhubiri alikuwa akizugumzia jambo ambalo mkalimani alikuwa analifahamu, huenda alipokosa kusikia viziri aliamua kujaliza kwa kutumia deta ya akilini. Kwa kufanya hivyo matatizo yakatokea katika ukalimani.

K5-4 Mhubiri: *Onge ng'ama oseneno Nyasaye kod wang'e.*

Mkalimani: "Hakuna mtu aliyemuona Mungu na uso".

Mkalimani aliteua neno ambalo halifai. Neno la Kiluo *wang'e* lina maana mbalimbali kwa kutegemea muktadha ilimotumiwa. Linaweza kuwa na maana ya 'uso', au 'macho' na kati ya maana hizo, maana iliyofaa katika muktadha huo ni macho. Watu huona kwa kutumia macho lakini hukutana uso kwa uso. Uteuzi wa neno uso kwa hiyo haukufaa kwani neno hilo lingeleta tatizo la kimantiki.

K5-8 Mhubiri: *Kar mondo olam Nyasaye*

Mkalimani: "Badala ya kumuomba Mungu"

Uteuzi wa neno 'kumuomba' haukufaa na ulipotosha ujumbe wa mhubiri. Jambo ambalo mhubiri alikuwa akizungumzia ni kule kuabudu vitu vingine mbali na Mungu. Ni kweli kwamba *olam* ina maana ya 'kuomba' lakini pia ina maana ya 'kuabudu'. Katika muktadha huo ingekuwa bora zaidi kama mkalimani angetumia neno 'kumuabudu' badala ya 'kumuomba'.

K5-11 Mhubiri:*Kata yande ochulo skul fis ni nyithindo*

Mkalimani: "Hata alipokuwa analipa mahari kwa watoto wa shule".

Mkalimani alitumia leksia ambazo hazifai katika sehemu hii. Huenda hangeweza kukumbuka neno lililofaa kwa haraka ambalo lilikuwa ni 'karo' na badala yake akatumia 'mahari'. Mahari hulipwa kwa mtu anayeolewa. Kwa hivyo hakuna njia yoyote ambayo mahari yangelipwa kwa watoto wa shule. Watu ambao hawaelewi Kiluo huenda walifikiria kuwa mhubiri alikuwa akisema kwamba watoto wanalipiwa mahari wakiwa wangali shuleni .Tunaamini hilo lilisababisha matatizo na hali ya kutoeleweka kwa sababu hayo hayakuwa makusudio ya mhubiri.Alisema kuwa hata kama alikuwa akilipa karo kwa motto wa shule anaanza kupuuza jukumu hilo.

K6-11 Mhubiri:....*mich mar dolo*

Mkalimani:..talanta ya unabii.

Mkalimani alitumia neno ambalo halina maana sawa na lile neno ambalo mhubiri alitumia.Neno *dolo* lina maana ya 'ukuhani' na wala si 'unabii'. Maneno hayo yana maana tofauti katika Biblia hivi kwamba matumizi ya moja badala ya jingine husababisha matatizo katika kuelewa ujumbe unaowasilishwa.

K6-19 Mhubiri:..*ka duong' mar Nyasaye onge*

Mkalimani:..kama ufalme wa Mungu hakuna.

Katika sehemu hii mkalimani alitumia neno ambalo halifai. Neno *duong'* linamaanisha utukufu lakini mkalimani alitumia neno 'ufalme' badala yake. Jambo hilo lingeweza kuleta matatizo katika kuelewa ujumbe wa mhubiri.

Kwa mujibu wa mifano hiyo tuliyotoa hapo juu, imebainika kwamba uteuzi wa kifasiri kifaacho hutekelezea jukumu kubwa katika kuwasilisha ujumbe sahihi wakati wa ukalimani. Jambo hili ni muhimu, hata zaidi, wakati wa kubadilisha ujumbe kutoka lugha ambayo neno moja linaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Katika hali kama hiyo, uteuzi kimantiki unafaa

upewe uzingativu mkubwa la sivyo, ujumbe utakalimaniwa visivyo kama ilivyotokea katika ukalimani kati ya lugha ya Kiluo na lugha ya Kiswahili.

Kutokuwa na msamiati wa kutosha wa lugha pia kulisababisha matatizo katika ujumbe. Viashiria vya dai hilo ni katika mifano ambayo mkalimani alishindwa kutumia kifasiri kifaacho ilihali kifasiri hicho kipo katika lugha lengwa.

Mifano hiyo ilitufanya kuelewa ni kwa nini Nida alisizitiza kwamba ili mtafsiri afanye kazi nzuri, ni sharti afahamu lugha zote mbili kama lugha mama . Ilibainika kwamba kati ya wakalimani wote tuliowachunguza, hakuna hata mmoja ambaye alifahamu lugha zote mbili kama lugha mama lau sivyo, matatizo hayo hayangetokea.

### 4.4.3 Matatizo Anuwai.

Kuna matatizo mengine ambayo yalijitokeza wakati wa ukalimani ambayo licha ya kutokuwa ya kisintaksia wala kileksia yalileta matatizo katika ujumbe wa lugha lengwa.

Baadhi ya matatizo haya ni kama vile matumizi ya maneno yaliyoazimwa kutoka lugha nyingine ambayo si lugha chanzi wala lugha lengwa. Kwa mfano, kuna wakalimani ambao walikuwa wakibadilisha maana kutoka Kiingereza hadi Kiluo; lakini, katika baadhi ya sehemu walitumia Kiswahili. Jambo kama hili lilichukuliwa kwamba ni tatizo la kuchanganya ndimi. Hakukuwa na ishara kwamba waliolengwa walikuwa na weledi wa lugha hiyo mpya.Tumedondoa mifano kadhaa ili kuonyesha mahali ambapo jambo hilo lilitokea.

Pia, kulikuwa na sehemu ambazo wakalimani walipuuza sehemu zingine na hata kuleta matatizo katika ujumbe kwa kusema maneno au kuwasilisha dhana tofauti kabisa na yale ambayo mhubiri alikusudia. Katika baadhi ya sehemu hizo, mkalimani alifanya hivyo ili kutia chumvi yale ambayo mhubiri alisema.Mifano ifuatayo itadhihirisha dai hili.

K1-7 Mhubiri: *The spirit of the living God began speaking to me.*
Mkalimani: *Roho mar Nyasaye nochako wuoyo koda.*

Tafsiri ya neno *spirit* kuwa 'roho' tayari tumeshugulikia katika sehemu ya leksia. Hata hivyo, katika sehemu hiyo mkalimani alipuuza neno *living*. Neno hilo living hutumiwa katika dini hasa ya Kikristo kuonyesha uwezo wa Mungu . Itaonekana hapa kwamba wakati neno hili linapowasilishwa katika maandishi Mungu huandikwa kwa herufi kubwa. Katika usemi jambo

hili haliwezekani. Wahubiri wengi hupenda kutumia neno hilo *living* kuonyesha tofauti kati ya miungu iliyochongwa ambayo huabudiwa katika baadhi ya imani. Neno hilo kwa hiyo lilikuwa na umuhimu mkubwa. Kulipuuza kuliweza kusababisha tatizo katika kuelewa ujumbe uliokalimaniwa.

K1-17 Mhubiri: *I am a Baptist.*

Mkalimani: *Ne otisa.*

Ukalimani uliofanywa hapa ni mfano wa kuwasilisha dhana ambayo mhubiri hakukusudia kuwasilisha. Katika sehemu hiyo mhubiri alikuwa akijaribu kueleza jinsi wakristo walivyogawanyika katika madhehebu mbalimbali. Wengine wakisema kuwa mimi ni 'mbaptisti'. Mkalimani akatafsiri kuwa mimi nilibatizwa ambayo ndiyo maana ya *ne otisa.* Ukalimani huo ulileta maana tofauti. Mhubiri hakumaanisha yale yaliyosemwa na mkalimani. Mkalimani alifaa aseme *an ja Baptist.*

K1-23 Mhubiri: *Will you stand and say love thy God with all thy heart.*

Mkalimani: *Anachung' mi awachi ni her Nyasaye gichunyi duto.*

Katika sehemu hii mkalimani alibadilisha nafsi.Mhubiri alitumia nafsi ya pili lakini yeye akatumia nafsi ya kwanza. *Anachung'* badala ya *inichung'* Mhubiri alisema kwa kuuliza swali "utasimama na kusema, mpende Mungu wako kwa moyo wako wote?".
Mkalimani kwa upande mwingine alisema "nitasimama na kusema mpende Mungu wako kwa moyo wako wote". Ingawa Mhubiri alionekana kuwa anauliza swali, swali hili halikujitokeza katika ukalimani. Kile kilichojitokeza ni kuwa mkalimani alionekana kuwa anajibu swali hilo la mhubiri. Kule kubadilisha nafsi kumesababisha matatizo hivi kwamba swali ambalo hadhira iliulizwa ambalo walitarajiwa kujibu halikuwafikia.

K1-26 Mhubiri: *It is not who will be critical first.*

Mkalimani: *Ok en ng'ama noher mokuongo.*

Katika sehemu hii mhubiri alikuwa akieleza kuwa watu wanapoenda mbele ya hakimu, anayetoa uamuzi hatazingatia tu yale yanayosemwa na yule atakayekuwa wa kwanza kumshtumu au kumshtaki mwenzake. Mkalimani amesema "si yule anayependwa kwanza". Ni wazi hapa kwamba mkalimani alitoa tafsiri ambayo ni tofauti kabisa na yale ambayo mhubiri alisema. Huenda hii tafsiri isiyo kamilifu ilitokea kwa sababu mkalimani hakusikia kile ambacho mhubiri alisema ama kama alisikia hakuelewa. Pengine lingekuwa jambo la busara kama angemuomba mhubiri arudie maneno yale ili ayapate sawa sawa. Kutofanya hivyo kumesababisha hali ambayo wanaokalimaniwa wamepata maneno mengine tofauti sana na yale ya mhubiri. Angesema *ok ng'ama okuongo donjo niwadgi.*

K2-6 Mhubiri: *continue my love.*
Mkalimani*: dhiuru mbele gi herana.*

Katika sehemu hii ukalimani karibu wote ni sawa isipokuwa matumizi ya neno la Kiswahili "mbele". Msimamo wetu ni kwamba hakuna haja ya kuleta lugha nyingine ya tatu pasipo na sababu maalum. Ni muhimu kusisitiza hapa kwamba kuna neno la Kiluo "*nyime*" ambalo lina maana ya mbele. Kama hakungekuwa na neno la Kiluo, basi ingeeleweka ni kwa nini ameingiza neno kutoka lugha nyingine. Hata akiingiza neno kama hilo katika ukalimani wake, linafaa liwe neno ambalo wale wanaokalimaniwa tayari wanalifahamu kama tulivyoona katika Roho Mtakatifu hapo awali. Kama tulivyosema hapo awali, matumizi ya lugha tofauti katika ukalimani huweza kusababisha matatizo iwapo wanaokalimaniwa hawaelewi hiyo lugha ya tatu.

K2-37 Mhubiri: *God want's to take the diversity of thy struggle.*
Mkalimani*: Nyasaye dwaro mondo okaw okang' mar thuthni ni.*

Katika sehemu hii mhubiri alitumia msemo wa Kiingereza ambayo ina maana ya kupigana kwa niaba ya mtu mwingine. Mkalimani hakuelewa maana ya msemo huo na kwa hiyo ukalimani aliyotoa ni "achukue hatua za juhudi zako" badala ya "apigane kwa niaba yako". Kutoelewa msemo huo kulisababisha matatizo kwa sababu tafsiri ya mkalimani haikuwa sahihi. Angesema *Nyasaye dwaro mondo oked e loyi.*

K2-42 i Mhubiri: *The spirit will spill in you.*

Mkalimani:.....

Sehemu hii yote ilipuuzwa na mkalimani. Kupuuzwa kwa sehemu yoyote ile kwa sababu yoyote kunasababisha matatizo ya kuvunja mtiririko wa kimantiki wa ujumbe wa Mhubiri na kufanya sehemu inayofuata kutoeleweka vyema.

K2-42 ii Mhubiri: .... *by finding the part of the bible that you left on the ground.*

Mkalimani*: ka iyudo part mar muma mane iweyo e lowo.*

Katika sehemu hii mkalimani alitumia neno la Kiingereza *part* moja kwa moja bila kulifanyia marekebisho yoyote au kufanya juhudi zozote za utohozi. Mbinu hiyo ni kuchanganya ndimi. Kufanya hivyo kulikuwa sawa na kuchukulia kwamba hadhira yake ilielewa lugha ya Kiingereza. Ikiwa waliohudhuria walielewa lugha zote mbili basi hakukuwa na haja ya kuwa na ukalimani katika mkutano huo. Tulichukulia kwamba ikiwa kulikuwa na watu katika hadhira ambao hawaelewi lugha ya Kiingereza, watu hawa hawakuelewa sehemu hizo zilizokuwa na lugha ngeni. Kwa watu hawa, kutumia neno la Kiingereza moja kwa moja kulikuwa sawa na kuacha nafasi katika sehemu hiyo na kuifanya ama kutoeleweka au kueleweka visivyo. Tukio kama hilo katika ukalimani husababisha matatizo katika ujumbe wa ukalimani.

K3- 1 ii Mhubiri: *we glorify your name our living father.*

Mkalimani: *wating'o nyingi sani.*

Mkalimani ametafsiri tu sehemu ya sentensi hiyo " tunalitukuza jina lako" na kupuuza sehemu ya *Our living father*. Kama tulivyotangulia kusema, lugha ya kidini ni lugha maalum ambayo Mungu ana sifa zake za kipekee. Sifa hizo za Mungu zinaonyesha uwezo wake. Kupuuza baadhi ya sifa hizo wakati wa ukalimani kunaweza kuathiri imani ya hadhira kuhusu uwezo wa Mungu. Katika mfano huo, ni kama vile Mungu yu hai tu katika lugha ya Kiingereza na wala si katika lugha ya Kiluo. Ukalimani kama huo, kwa hiyo unaweza kuleta matatizo. Hapo angesema *Wamiyo nyingi duuong' Nyasaye mangima;* yaani 'tunakutukuza Mungu ulie hai'.

K3-1 iii Mhubiri: *Lord have mercy upon every soul that is here.*

Mkalimani: *Jehova Nyasaye tim ng'uono.*

Katika sehemu hiyohiyo, mkalimani alipuuza sehemu inayosema *Upon every soul that is here.* Hii ina maana kuwa alianzisha kile ambacho mhubiri alisema lakini hakukikamilisha. Ingawa wanaoelewa Kiingereza walipata kila kitu, wale wanaoelewa Kiluo peke yake wamepata nusu tu. Ile sehemu iliyopuuzwa ni muhimu sana kwa hadhira hiyo kwa sababu ndiyo inaweka ombi hilo katika muktadha wao.

K3-2 Mhubiri:.... *as we continue praising you God.*

Mkalimani: ....*ka wadhi mbele*.....

Hapa kuna matatizo mawili. Tatizo la kwanza ni kwamba mkalimani ametumia neno la Kiswahili "mbele" na hivyo kuingiza lugha ya tatu katika mkutano huu.

Neno mbele lina kifasiri chake katika Kiluo nacho ni *nyime* na kwa hiyo mkalimani hakuwa na sababu mwafaka ya kuingiza Kiswahili. Tatizo la pili ambalo ndilo lilisababisha matatizo zaidi ni kwamba mkalimani hakupewa muda wa kukamilisha kukalimani maneno ya mhubiri.

Alifasiri tu hadi *as we continue* halafu mhubiri akadakiza na hivyo kumkatiza mkalimani. Kumkatiza mkalimani kulikatiza ujumbe kwa sababu maneno ya mhubiri hayakuwafikia yote.

K3-6 ii Mhubiri: *He wants to know you*

Mkalimani: *Entie gi gimomiyo*

Ukalimani huo umetengana kimaana na yale ambayo mhubiri alisema. Mhubiri alisema 'anataka kukujua au kukufahamu' lakini mkalimani alitoa tafsiri ambayo ina maana ya 'ana sababu'. Tulifikiria kwamba huenda mkalimani hakusikia yale ambayo mhubiri alisema. Badala ya kumuuliza kurudia, aliendelea na kutoa tafsiri zenye matatizo . Ilitakikana aseme *Odwaro ng'eyi.*

K3-9 Mhubiri: *In the community where we are in today*

Mkalimani: *E gweng' kata kuonde ma wadakie*

Huu ni mfano wa ukosefu wa maelewano kati ya mhubiri na mkalimani. Katika sehemu hii mhubiri alikuwa akijaribu kueleza kwamba miongoni mwa waluo, kuna vitendo ambavyo huonyesha heshima.Aliposema *In the community where we are in today* alimaanisha hapa mahali tupo ama watu hawa tunaowahubiria. Tafsiri ya mkalimani ina maana ya *In the villages where we live* ambao inaleta maana ya jumla. Itikadi hiyo ya waluo ambayo alinuia kueleza haijitokezi katika vijiji vyovyote vile bali hutokea miongoni mwa watu wa jamii hiyo. Tatizo lilitokea kwa sababu mkalimani hakuelewa yale ambayo mhubiri alikuwa akisema. Alitoa maelezo ambayo yana maana tofauti kabisa

K3-10 Mhubiri: *You must put on the head and the legs*

Mkalimani: *Nyaka ikaw wi gwenono*

Mkalimani alisababisha tatizo hapa kwa sababu hakueleza yale ambayo mhubiri alitaka kusema.

Mhubiri alikuwa akijaribu kueleza kuwa miongoni mwa jamii ya waluo, mgeni anapochinjiwa kuku, lazima apakuliwe kichwa cha kuku kama ishara ya heshima. Mkalimani alisema tu 'lazima uchukue kichwa cha kuku huyo' hakusema kichwa hicho kinafanywaje na kwa hiyo waliokalimaniwa hawakupata ujumbe wa mhubiri. Swala kiyamaduni ambalo mhubiri alikuwa na nianya kueleza halikujitokeza bayana hapa.

K3-12Mhubiri:This is the hour to acknowledge your God

Mkalimani: *Ma e thuolo……*

Kilochotokea hapa ni kwamba mkalimani alitafsiri hadi *This is the hour* yaani 'Huu ndio wakati' na kuacha sehemu zingine kuanzia '*to* ……..mpaka *your God.'* Jambo hilo lilitokea kwa sababu mhubiri alikuwa akiongea harakaharaka bila kumpa mkalimani nafasi ya kukamilisha maneno yake yaliyotangulia. Mkalimani alipokuwa akikalimani, mhubiri alianza kuongea na katika kujaribu kusikia yale ambayo mhubiri alikuwa akisema huku akikalimani, alikanganyika na kuachia sentensi hiyo katikati bila kuikamilisha. Jambo hilo lilisababisha tatizo kwa sababu sehemu hiyo ilipuuzwa. Iliacha pengo katika maneno ya mhubiri na kuwafanya wale wanaoelewa Kiluo peke yake kupata tu nusu ya maneno waliyokusudiwa.

K3-15 Mhubiri : *It doesn't matter the situation you are in*

Mkalimani: *Ok odewo hali ma intie*

Mkalimani alitumia neno 'hali' ambalo ni neno la Kiswahili. Kama mkalimani alikuwa makini pamoja na kuwa na weledi wa kutosha wa lugha ya Kiluo angesema *'ok odewo kaka ichal'* badala yake mkalimani ameleta neno 'hali' ambalo huenda watu wengi katika hadhira hiyo hawakulielewa. Ikiwa wale wanaokalimaniwa hawaelewi sehemu yoyote ile ya ukalimani, basi hali hiyo husababisha matatizo.

K4-1 Mhubiri : *Kendo mobedo gi hero kuom winjo*

Mkalimani: .....

Mkalimani alipuuza sehemu hiyo yote ambayo ina maana ya "ambao wanafurahia kusikia". Haikueleweka mkalimani alipuuza sehemu hiyo kwa nini. Lakini sehemu hiyo ilikuwa muhimu kwa sababu alikuwa anamwomba Mungu kuwabariki wote wanaosikia vizuri. Wale waliohudhuria na ambao wanaelewa lugha ya Kiswahili pekee hawakupata maneno haya.

K4-3 Mhubiri: *Kane oseduokogi penjo manechandogino*

Mkalimani: Alipokuwa akiwajibu swali hilo.

Mhubiri alitumia wakati uliopita. 'Baada ya kuwajibu swali hilo'. Mkalimani kwa upande wake alitumia wakati uliopo hali ya kuendelea. Uchaguzi huu mbaya wa njeo kwa upande wa mkalimani ulisababisha tatizo. Kile kilicholeta amani mioyoni mwa wale waliokuwa wakimsikiza Yesu ni jawabu alilotoa. Ikiwasilishwa katika hali ya kuendelea, maana inayojitokeza ni kwamba 'mioyo ya watu hao ilitulia hata kabla Yesu hajamaliza kuwajibu'. Maana kama hiyo humpa Yesu sifa ambazo hazipo katika msahafu. Huku ni kutia chumvi katika neno la Mungu.

K4-4 i Mhubiri : *Otiyo matek to ok one ka en kod ngima*

Mkalimani: Anafanya jambo moja lakini haoni kama ana amani.

Hapa mkalimani hakusema yale ambayo mhubiri alisema yaani- 'Anaweza kuwa na bidii lakini haoni kama ana uzima'. Mkalimani kwa upande wake akasema 'anafanya jambo moja

lakini haoni kama ana amani'. Maana ya vifungu hivyo viwili ni tofauti kabisa. 'Bidii' ni tofauti na 'kufanya jambo moja'. Kwa vile 'uzima' na "amani" ni mambo mawili tofauti, waliohudhuria ambao hawaelewi Kiluo walipata maana tofauti na wale wanaoelewa Kiluo. Hili tatizo huenda lilitokea kwa sababu ya ukosefu wa makini kwa upande wa mkalimani.

K4-5 Mhubiri : *wachno en adiera pile kata e dala maru ka.*

Mkalimani : jambo hilo ni kweli tena lina uzima katika mji huu.

Ingawa mkalimani amewasilisha maneno yote ambayo mhubiri alisema, tatizo hapa ni kwamba ameongeza maneno yake mwenyewe 'tena lina uzima'. Si jambo jema kwa mkalimani kuongeza maneno yake mwenyewe kwani kufanya hivyo ni sawa na kubadilisha ujumbe wa mhubiri. Anapofanya hivyo ujumbe unakuwepo mara mbili. Ule wa mhubiri na ule wa mkalimani. Mkalimani ni mkalimani na si mhubiri . Kwa hivyo, ni vyema asiruhusu hisia zake za kibinafsi kuingilia ujumbe wa mhubiri kwa kuingiza maneno yake mwenyewe.

K4-8 Mhubiri: *...ka yo be osetami*

Mkalimani... kama umekosa umeshindwa.

Mhubiri alisema 'kama njia imekushinda' lakini mkalimani alisema 'kama umekosa umeshindwa' maneno haya ya mkalimani hayana maana sawa na yale ambayo mhubiri alisema. Hayana maana yoyote katika muktadha wa mahubiri yaliyokuwa yakiendelea. Huu ni mfano wa mkalimani anayekalimani bila kujali athari ya maana kwa mujibu wa muktadha. Athari yake ni mbaya sana kwa wale wanaokalimaniwa. Kwa mfano katika sehemu hiyo, sehemu ya hadhira wanaoelewa Kiswahili peke yake hawakupata chochote.

K4-12 Mhubiri: *gik ma Nyasaye timo ni joge*

Mkalimani : yale ambayo Mungu anataka.

Mhubiri alisema 'Yale ambayo Mungu anawatendea watu wake' Mkalimani alisema 'Yale ambayo Mungu anataka' Mkalimani alipotosha ujumbe huo kwa kuleta dhana ambayo haikuwepo katika maneno ya mhubiri.

Hapa pia tulifikiria kwamba matatizo haya yalitokana na ukosefu wa makini kwa upande wa mkalimani na kwa mara nyingine wanaoelewa Kiswahili pekee hawakupata ujumbe wa mhubiri.

K5-5 Mhubiri : *Mana kaka nochung thuond mula e thim*

Mkalimani: Vile lile joka lilisimamishwa jangwani

Joka ambalo mhubiri alikuwa akizungumzia halikuwa joka la kweli. Ni joka lililotajwa katika Biblia ambalo Musa aliamriwa kulitengeneza kwa kutumia madini ya shaba. Mhubiri kwa hivyo alisema *thound mula* kumaanisha 'joka la shaba' lakini mkalimani alisema tu 'joka'. Huenda waliosikiza walifikiria kuwa mhubiri alikuwa akizungumzia joka lingine mbali na lile la shaba. Kwa kupuuza neno 'shaba' mkalimani alifasiri visivyo ujumbe wa lugha chanzi.

K5-6 Mhubiri :... *ka dibed ni nitie jomoko ma ok oyudo ngimano*

Mkalimani :... yaweza kuwa kuna wengine wakipata huo uzima.

Mkalimani alisababisha tatizo katika ujumbe wa lugha lengwa kwa kutumia neno'wakipata' badala ya neno 'hawajapata'. Neno 'wakipata' linaingiza masharti katika kifungu hicho ilhali yale ambayo mhubiri alisema yalikuwa yakinishi. Sharti hilo lililoingizwa na mkalimani lilifanya sehemu hiyo kuhitaji maelezo zaidi kutoka kwa mnenaji. Kutotolewa kwa maelezo hayo kunaifanya sehemu hiyo kutoeleweka.

K5-15 Mhubiri:... *nikech gilal e ndawa*

Mkalimani: ...kwa sababu wamepotelea bangi.

Tulichukulia kwamba mkalimani aliupotosha ujumbe wa mhubiri makusudi ili kujaribu kurekebisha ujumbe huo. *Ndawa* ni sigara. Tunaamini kwamba mkalimani anajua vizuri sana tofauti kati ya sigara na bangi.Pengine alifanya marekebisho hayo kwa sababu maneno ya mhubiri yaliyotangulia yalisema kuwa 'wengine wameshikwa na serikali'.

Mhubiri aliposema kwa sababu wamepotelea sigara, mkalimani pengine aliona kuwa kimantiki, mtu hawezi kushikwa kwa sababu ya sigara, badala ya kutumia neno sigara akatumia

neno bangi. Huu ni ukalimani usiofaa kwa sababu mkalimani hawezi kujua kuwa mhubiri aliposema hayo alikuwa na maana gani. Upotevu ungeweza kumaanisha wizi wa sigara, au wizi ili kununua sigara. Marekebisho hayo ambayo mkalimani alifanya kwa hivyo hayakustahili. Hayo ni baadhi ya mambo ambayo Peterson alizungumzia ambayo yamo katika sehemu yetu ya yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.

### 4.4.4. Matatizo ya Kisintaksia.

Katika sehemu hii, tulizingatia sehemu ambazo matatizo ya aina hii yalitokea. Tulidondoa sehemu zenyewe pamoja na ukalimani wake na kisha kutoa maelezo kuhusu jinsi tulivyofikiria ukalimani huo ulisababisha kueleweka visivyo kwa ujumbe: -

K1-29 Mhubiri*: There is a dying world that needs the same love.*

Mkalimani*: Nitie piny matho modich gi hera nogo.*

Mkalimani alisema kwamba ' kuna dunia inayokufa ambayo inahitaji upendo huo' kisemantiki tafsiri hii haina maana yoyote. Tatizo hili limetokea kwa sababu mkalimani aliwania kutafsiri maneno ya mhubiri pamoja na muundo wa sentensi yake vile ilivyokuwa. Angesema *nitie ji matho madwaro hera* ili iwe na maana ile ya mhubiri. Kile ambacho mhubiri alikuwa akisema ni kwamba kuna watu wanaokufa ambao wanahitaji upendo. Dunia haiwezi kuhitaji upendo. Katika Kiingereza maana ya usemi huo inajitokeza wazi kwa sababu '*world*' katika muktadha huo inamaanisha watu. Lakini ikitafsiriwa moja kwa moja katika Kiluo vile alivyofanya mkalimani maana inapotea.

K1-31 Mhubiri*: Does one ever wake up at night and see the sky*?

Mkalimani*: Be ng'ato nyalo chiew gotieno mi one polo.*

Hii ni tafsiri ya sisisi, neno kwa neno pamoja na muundo. Tatizo ni kwamba ikiwa maneno hayo yameachwa katika muundo huohuo, maana iliyokusudiwa na mhubiri haijitokezi. Maana inyojitokeza ni: -

'Mtu anaweza kuamka usiku na kuangalia mbingu?'angesema *"be ngato osechiew gotieno mi ong'iyo polo?"* Mhubiri alikuwa akiuliza kama watu wamewahi kutoka nje usiku na kutazama mbingu.

Licha ya kwamba maneno yaliyokuwemo katika maneno ya mhubiri yametafsiriwa yote, ujumbe uliomfikia mpokezi una matatizo kwa sababu ya kutopangwa upya kwa muundo wa tungo ufaao.

K2-2 i Mhubiri*: God desires that we should have his likeness.*

Mkalimani*: Nyasaye dwaro ni mondo wabed gi chalne*

Tafsiri hii vilevile ni ya moja kwa moja ambapo maneno yaliyomo katika lugha chanzi yamehamishwa vile yalivyo. Katika ukalimani, sintaksia ya lugha chanzi pia imebakia vile vile. Matokeo yake ni kwamba mklimani alipofikia mwisho wa sentensi hiyo, Ilimbidi atumie neno ambalo halielezi maana ambayo mhubiri alidhamiria . Neno '*chalne*' lina maana ya ' mfanano wake'. Katika lugha ya Kiluo neno hilo katika muktadha huo halina maana. Maneno ' *mondo wachal kode'* ndiyo yangefaa zaidi yaani ' tufanane naye'. Hata hivyo mkalimani hangeweza kutumia maneno hayo pamoja na sintaksia hiyo; kwa hiyo, sintaksia isiyofaa imemlazimisha kutumia neno lisilofaa na hivyo kusababisha matatizo katika ujumbe.

K2-2 ii Mhubiri: *You have a beautiful place*

Mkalimani*: Un gi kama ber*

Katika juhudi ya kuhifadhi sintaksia hiyo ya lugha ya Kiingereza, mkalimani ametafsiri moja kwa moja. Kulingana na muktadha wa usemi huo wa mhubiri, nchi ya Kenya ni nzuri. Maneno hayo yakitafsiriwa neno kwa neno vile mkalimani alivyofanya, dhana ambayo inajitokeza ni ' mko na mahali pazuri' ambayo si sawa na kusema ' nchi yenu ni maridadi'. Jaribio la kuhifadhi sintaksia ya Kiingereza kwa hiyo limemfanya mkalimani kutumia maneno yaliyosababisha matatizo katika ujumbe wa lugha chanzi.Angesema *"un gi piny maber"*

K2-29 Mhubiri: *My brother here have the issue.*

Mkalimani: *Owadwa nigi wachno.*

Mkalimani amefuata sintaksia ya Kiingereza ; kwa hivyo, kutumia maneno ambayo licha ya kuhifadhi sintaksia hiyo, yameibadilisha au kuleta matatizo katika maana ya usemi wa mhubiri. Mhubiri alikuwa akieleza kuwa huyo mwenzake ambaye alikuwa ameketi karibu naye anafahamu tukio alilokuwa akitoa maelezo yake. Kutafsiri kwa kusema '*owadwa nigi wachno*' ni sawa na kusema 'huyu ndugu yangu ana jambo hilo.' Hata katika Kiswahili ni vigumu kuelewa anachomaanisha, mtu anaposema ' ana jambo hilo'ingefaa zaidi kama angesema, "*owadwa ni ong'eyo wachno.*"

K3-4 Mhubiri: *That is why he is here in Bondo.*

Mkalimani: *Mano emomiyo entiere kae Bondo.*

Katika sehemu hii mkalimani vilevile ametumia sintaksia ya Kiingereza . Ingawa yale anayosema yanaweza kueleweka, tafsiri hiyo ni sawa na ya mtu anayejifunza lugha ya Kiluo kwa mara ya kwanza au mtu ambaye lugha ya Kiluo si lugha yake asilia.Katika Kiluo neno *kae* lilifaa kuachwa nje ndipo tafsiri hiyo ingekuwa sawa ,kisarufi. Ingekuwa bora zaidi kama angesema "*mano emomiyo en Bondo .*"

K3-8 Mhubiri: *To share it with other people*

Mkalimani: *Wapoge gi jomoko*

Mhubiri aliposema hivyo alimaanisha watu wanaweza kuwaambia wengine kuhusu neno la Mungu. Hiyo ndiyo maana ya neno la Kiingereza ' *share*' katika muktadha huo. Mkalimani hata hivyo alichukua neno hilo kwa maana ya 'kugawanya' na kuleta maana ya 'kuligawanya na watu wengine". Hapo mambo mawili yametokea; Kwanza ni lile la kihifadhina juu ya sintaksia na pili ni kuteua neno lisilofaa ili kumsaidia kuhifadhi sintaksia hiyo ya Kiingereza. Watu hawawezi kugawanya neno na wengine bali huwaambia neno. Angesema *wawachne jomoko.*

K5-1 Mhubiri: *Nyasaye nigi tiende kuom kelowa ka.*

Mkalimani: *Mungu ako na mguu kwa kutuleta hapa.*

Mkalimani aliwania kufuata muundo wa sentensi hiyo vile ilivyokuwa. Katika kufanya hivyo ametafsiri maneno ya mhubiri vile yalivyo bila ya kuyafikiria kwa makini wala kuelewa yale ambayo mhubiri alikuwa akisema.Mkalimani hakuzingatia muktadha. Maneno hayo ya mkalimani ndiyo tafsiri ya moja kwa moja ya kifungu hicho cha Kiluo. Ukalimani huo hauna maana hivi kwamba anayeelewa lugha ya Kiswahili hawezi kufahamu kile ambacho msemaji anamaanisha. Katika lugha ya Kiluo neno *' tiende'* lina maana tatu.

(a) Maana

(b) Sababu

(c) Mguu

Uteuzi wa neno mguu haukufaa kimantiki. Uteuzi huo umesababisha tatizo la kimantiki lililotokana na muundo wa sentensi hiyo..Maana ambayo mhubiri alikusudia ni kwamba 'Mungu ana sababu za kutuleta hapa'.

K5-5 Mhubiri: *Wach moro nitie ni ngima*

Mkalimani: *Neno lingine liko kwamba ni uzima.*

Katika tafsiri hiyo mkalimani amebadilisha maneno yote kwa kufuata muundo wa Kiluo. Muundo huo hauleweki katika lugha ya Kiswahili iwapo hakuna marekebisho ya kisintaksia yaliyofanywa. Katika kifungu hicho mhubiri alisema kwamba ' kuna jambo liitwalo uzima' Mkalimani kwa hiyo ameishia katika kuleta matatizo katika ujumbe huo wa mhubiri na kufanya fasiri yake ya Kiswahili kutoeleweka.

K5-6 Mhubiri: *Nitie weche moko mopondo ne dhano*

Mkalimani*: Kuna mambo mengine yaliyojifichia binadamu*

Katika mfano huu pia, ingawa mkalimani alijaribu kutafsiri maneno yote ambayo yamo katika tamko la mhubiri, ukalimani wake haueleweki kwa mzungumzaji wa Kiswahili. Hii imetokana na kujaribu kufuata muundo wa kisarufi wa Kiluo huku akibadilisha maneno katika

Kiswahili kwa kuteua vifasiri sahihi kadri iwezekanavyo. Mhubiri alikuwa akisema kwamba ' kuna mambo ambayo binadamu haelewi'. Katika sentensi hii tunaona kwamba kwa kubadilisha muundo wa sentensi na kuweka neno binadamu katika nafasi ya mtenda, sentensi hiyo ingeeleweka vizuri.

K6-13 Mhubiri:*Oonge gi pek mar lando wach.*

Mkalimani:Hana mzigo wa kuhubiri neno.

Hapa mkalimani ametumia tafsiri ya neno kwa neno. Neno ambalo mkalimani ametafsiri kuwa mzigo lingefaa liwe ari yaani hana ari ya kutangaza neno

Kwa mujibu wa mifano hiyo tuliyoitoa, imebainika kwamba sintaksia hutekeleza jukumu muhimu katika kufanikisha mawasiliano ya ukalimani hasa katika lugha mbili ambazo zina miundo tofauti ya kisarufi kama vile Kiluo na Kiingereza au Kiluo na Kiswahili. Kama tulivyobainisha hapo juu, mkalimani ambaye hutafsiri neno kwa neno mbali na kutumia maneno yasiyofaa, wakati mwingine pia huhamisha muundo wa sintaksia ya lugha chanzi hadi katika lugha lengwa.

Jambo hilo likitokea, inakuwa vigumu sana kuelewa ujumbe huo katika lugha lengwa. Pia, katika uchunguzi wetu wa matatizo ya kisintaksia tulibainisha kuwa umaratokezi wa matatizo hayo katika jozi hizo za lugha zilizokalimaniwa, Kiingereza – Kiluo na Kiluo-Kiswahili ulikuwa karibu sawa.Hiyo inaonyesha kwamba jozi hizo za lugha zina tofauti karibu sawa za kimuundo.

### 4.4.5 Matatizo ya Kimazingira na Kitamaduni

Tulipoazimia kufanya utafiti huu, tulikuwa na nadharia tete iliyosema kwamba matatizo katika ujumbe katika mahubiri hutokana na tofauti za kitamaduni na kimazingira kati ya lugha zinazohusika. Kulingana na Nida(1964), matatizo yote ya mawasiliano katika tafsiri hutokana na tofauti za kitamaduni na kimazingira kati ya lugha zozote mbili zinazohusika.

sehemu moja tu ambayo tofauti ya utamaduni wa kijamii ilibainika na kusababisha matatizo ya kutoeleweka kwa ujumbe.

K1-30 Mhubiri*: I want to love this woman*

Mkalimani : *Adwaro hero dadani*

Katika ukalimani huo mfasiri alisema 'Nataka nimpende dada huyu' badala ya mwanamke huyu. 'Dada huyu' haina maana sawa na 'mwanamke huyu'. Mkalimani alikuwa mtu wa umri mdogo akilinganishwa na huyo mke wa mhubiri ambaye alikuwa akirejelewa. Katika utamaduni wa waluo, mtu wa umri huo hawezi kutumia neno '*dhakoni'* ambalo ndilo lina maana ya mwanamke hadharani kumrejelea mwanamke wa umri aliyekuwa akirejelewa. Kufanya hivyo kungeonyesha ukosefu wa adabu.

Wanawake wa umri huo huitwa kwa majina ya watoto wao – yaani mama fulani au jina la kule alikotoka kama '*Nyagem*' na majina mengine bila kurejelea uana wake moja kwa moja. Licha ya hayo tatizo lilitokea kwa sababu kule kumwita dada hakukubainisha uhusiano kati yake na mhubiri. Waliohudhuria wangeweza kufikiria kuwa alikuwa dadake mhubiri badala ya mke wake.Huu ni mfano mzuri unaodhihirisha kuwa tofauti za kitamaduni za kijamii zinaweza kusababisha matatizo katika ukalimani.

### 4.4.6 Matatizo ya Lafudhi ya Mhubiri.

Lafudhi pia zilichangia katika kuleta matatizo katika ujumbe. Jambo lililobainika ni kwamba katika sehemu ambazo mkalimani hakusikia maneno ya mhubiri vizuri, aidha alipuuza sehemu hizo au aliweka neno ambalo halifai. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu, jambo hili lilisababisha matatizo hivi kwamba kulikuwa na mapengo hapa na pale kwa sababu ya kuachwa kwa sehemu zingine. Ujumbe hauwezi kueleweka vyema iwapo sehemu zake zingine zimeachwa nje. Sehemu ambazo mkalimani aliongeza maneno yake mwenyewe tayari zimeshughulikiwa upande wa leksia. Wawili kati ya wahubiri hao walitoka Marekani. Aliyekuwa akimkalimania mhubiri mmoja hakuwa amezoea lafudhi ya Kiingereza cha Kimarekani. Wakati moja mhubiri alisema:-

K1-1 Mhubiri : *My name is Blaine Rogers*

Mkalimani: *Nyinge en* ……

Mkalimani hakuweza kupata jina hilo la mhubiri hata baada ya mhubiri huyo kulirudia mara tatu. Hali hiyo ilikuwa mbaya zaidi katika kanda ya tatu. Katika kanda hiyo mkalimani aliacha sehemu nyingi bila ya kuzikalimani kwa sababu mhubiri alikuwa akiongea Kiingereza kwa lafudhi ambayo ilimtatiza.

**4.4.7. Matatizo ya Kasi ya Mahubiri.**

Kulikuwa na tatizo la wahubiri kutompa mkalimani muda wa kutosha kuweza kukamilisha maneno yaliyotangulia ya mhubiri kabla ya mhubiri kuendelea. Mhubiri katika kanda ya pili kwa mfano alikuwa akisema maneno mengi sana kabla ya kumpa mkalimani nafasi. Hata baada ya kumpa nafasi alikuwa akidakiza kabla ya mkalimani kumaliza.

Tatizo hilo pia lilionekana wakati mhubiri ambaye mahubiri yake yalinaswa katika kanda ya tatu alipokuwa akihubiri.

# SURA YA TANO
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa maelezo kwa ufupi kuhusu matokeo ya utafiti hasa kiini cha matatizo katika ukalimani, matatizo yaliyokumba utafiti, na hatimaye mapendekezo.

### 5.2.1 Muhtasari

Kwa mujibu wa uchunguzi tulioufanya tuliweza kugundua kwamba kulikuwa na matatizo katika kalimani za mikutano tuliyoichunguza. Matatizo hayo yalisababisha kutoeleweka vyema kwa ujumbe wa lugha chanzi katika lugha lengwa. Thibitisho lilitokana na maoni ya hadhira kuhusu ukalimani huo.

Kwa mujibu wa hayo , tuliweza kuthibitisha nadharia tete yetu ya kwanza kwamba wakalimani katika mikutano ya kidini ya Kikristo mjini Bondo wana matatizo katika kukalimani ujumbe wa lugha chanzi.

Tuliainisha matatizo au mambo yaliyosababisha matatizo katika ukalimani. Tulikuwa na nia ya kuzingatia hasa yale yaliyotokana na tofauti za kimazingira na kitamaduni kati ya lugha chanzi na lugha lengwa.

Ingawa katika uchanganuzi wetu itaonekana kwamba matatizo tuliyoyapata ni yale yaliyojikita katika isimu, inafaa ikumbukwe kwamba nadharia ya Nida ambayo ndiyo tulitumia katika utafiti huu inachukulia vipengele hivyo kuwa ni vipengele vya utamaduni hususan utamaduni wa lugha. Katika upande wa mazingira vilevile uchanganuzi wetu umeonyesha wazi kwamba vifasiri vilikosekana katika sehemu mbalimbali kwa sababu ya tofauti za kimazingira kati ya lugha zilizokuwa zikikalimaniwa. Kwa mfano katika sehemu ya Biblia ambayo Yesu alizungumzia ukulima na utunzaji wa mti wa mzabibu. Tofauti hiyo ilisababisha tatizo la kiisimu ya kutopata vifasiri vya kutumia katika lugha ya Kiluo hili ni tatizo la kileksia lakini kiini chake kilikuwa ni mazingira.

Katika upande wa utamaduni wa kijamii, tulipata ushahidi wa kutosha kuwa jambo hilo linaweza kusababisha matatizo katika ujumbe wa ukalimani. Utafiti huu kwa hiyo ulibainisha wazi kwamba kiini cha matatizo mengi katika ukalimani katika mikutano ya kidini mjini Bondo hutokana na matatizo ya kiisimu ambayo ni sehemu ya lugha. Kama tulivyoeleza hapo juu, kulingana na Nida(1964), yale mambo yanayohusu lugha ambayo tumezungumzia kama vile

sintaksia na leksia ni sehemu ya utamaduni wa jamii yoyote ile. Katika nadharia yake ya tafsiri mambo hayo yanakuja chini ya utamaduni wa lugha. Lugha ya jamii yoyote ile hutokana na mazingira yao ambayo ni sehemu ya utamaduni wao. Matatizo ya ujumbe katika kalimani za mahubiri katika mikutano ya kidini mjini Bondo, kwa hiyo, yalitokana na tofauti za kimazingira kati ya lugha zilizohusika katika ukalimani.

Kati ya wakalimani wote sita waliochunguzwa, hakuna hata mmoja aliyepata mafunzo yoyote kuhusu kazi ya ukalimani. Hiyo inathibitisha nadharia tete yetu ya tatu kwamba wakalimani hao hawajapata mafunzo yoyote. Hatuwezi kusema kwa uhakika kwamba jambo hili ndilo lilisababisha uhafifu wa utendaji kazi wao. Hii ni kwa sababu hatukupata yeyote aliyepata mafunzo ili tulinganishe wale ambao walikuwa wamepata mafunzo na wale ambao hawakuwa wamepata mafunzo. Ili kufikia uamuzi wenye uhakika kuhusu athari ya mafunzo ya wakalimani katika ukalimani, lazima kuwepo na ulinganishi kati ya waliopata mafunzo na wale ambao hawajapata mafunzo. Ulinganishi wa aina hiyo haungeweza kufanywa katika utafiti huu kwa sababu ya aina ya deta iliyotumiwa.

Nadharia ya Nida tuliyoitumia katika utafiti huu ulitusaidia katika kuainisha vipengele mbalimbali vya lugha ambavyo vilijenga msingi wa uchunguzi wetu. Ingawa vipengele hivyo yaani fonolojia, leksia, sintaksia na semantiki vinajulikana, kazi ya Nida ilitusaidia kuelewa vile vipengele hivyo vinahusishwa katika utamaduni wa lugha zozote zile. Maelezo ya Nida yalitusaidia kuelewa kwamba matatizo ya kiisimu tuliyogundua katika uchunguzi wetu yangeweza kueleweka kwa urahisi iwapo tunaweza kuangalia tofauti za kitamaduni na kimazingira kati ya lugha zozote mbili.

### 5.4. Mapendekezo

(i) Kabla ya mikutano ya kidini ya Kikristo ambayo ukalimani ungefanyika, ni muhimu kuwakutanisha mhubiri na mkalimani ili waweze kuzungumza, kufahamiana na hata kufahamishana sehemu ya Biblia ambayo mhubiri angesoma. Jambo hili linaweza kufanyiwa utafiti ili iweze kubainika kama linaweza kuboresha ukalimani.

(ii) Kuna haja ya wakalimani kutalii lugha zote mbili ili waweze kufahamu miundo yao pamoja na kufahamu maneno mengi kadri iwezekanavyo hasa yale ambayo hutumiwa katika Biblia. Jambo hili pia liambatishwe na kumfahamisha mkalimani sehemu ya Biblia ambayo mhubiri angesoma ili kumwezesha kuisoma katika lugha lengwa kama njia ya kujitayarisha ili istilahi iliyotumiwa katika Biblia isimtatize wakati anapofanya ukalimani.

(iii) Utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha kama wakalimani waliopata mafunzo wanaweza kufanya kazi bora zaidi katika mikutano kama hii kuliko wale ambao hawana mafunzo yoyote. Utafiti wa aina hii huenda ukasaidia kuamua iwapo wakalimani wa mikutano ya kidini wanafaa kupewa mafunzo au hapana na ni mafunzo ya aina gani ambayo yatawafaa.

(iv) Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi katika lugha mbalimbali katika maeneo mengine ili kubainisha matatizo zaidi na kupendekeza njia za kusuluhisha matatizo hayo.

(v) Kuna haja ya kurutubisha uwezo wa watafiti hasa upande wa nadharia. Nadharia nyingi zilizopo ni zile zinazohusiana zaidi na tafsiri.Iwapo nadharia mahsusi zitaibuliwa, basi huenda utafiti katika nyanja hii ya ukalimani ukarahisishwa.

(vi) Kwa vile istilahi inayofaa nyanja hii ni maalum, kuna haja ya wanaisimu kukubaliana juu ya istilahi muafaka zaidi katia Kiswahili kwa maneno yanayotumiwa kama vile transcription.

(vii) Ukalimani pia, hufanywa katika nyanja zingine kama vile mahakamni kufanikisha mawasiliano kati ya watu wanaohusika katika kesi mbalimbali.Utafiti ufanywe katika nyanja kama hiyo ili kuchunguza ufanisi wake , upungufu wake na njia za kuuboresha ukalimani huo.

## MAREJELEO


Anelo, C. G(2005) *Philosophy,Anthropology and Linguistics in translation: The Problem of Equivalence*.Proz.com journal.http//www.proz.com/284. 30/09/2005

Barker, M. (Ed) (1998*) Encyclopaedia of Translation Studies.* London and New York. Routeledge

Barker, M. (1992) *In Other Words: Course book on Translation* London Routeledge.

Bell, R.T(1991)*Translation and Translating Theory and Practice* London:Longman

Biguent, J. (1989) *The Craft of Translation (Chicago guides to Writing, Editing & Publishing)* Chicago Press.

Brown, R.L (1968*) Wilhelm Von Humboldts Conception of Linguistic Relativity* Paris: Mouton.

Brown, R. (1958*) Words and Things.* Illinois. The Free Press.

Catford, J.C. (1965) *A Linguistic Theory of Translation An Essay in Applied Linguistics.* London. Oxford University Press

Chandler, D. *Sapir Whorf Hypothesis.*http//www.aber.ac.uk/media/Documents/short/whorf.h.t.m 10/01/2005

Coulthard, M. (1977*) An Introduction to Discourse Analysis* London / New York Longman.

Cremona,V. and Mallia, H. (2004*) Language and Diplomacy Interpretation and Diplomacy.* Malta: Diplo projects

Crystal, D. (1987) *Cambridge Encyclopedia of Language.* Cambridge Cambridge University Press.

Duranti, A. (1997) *Linguistic Anthropology*. Los Angeles, Cambridge University Press.

Fram-Cohen, M.(1985)Reality Language Translation.*What Makes translation possible*.American Translators Association conference.Miami.http//enlightenment.supersaturated.com.

Kraft, H. (1979) *Christianity in Culture. A study in Dynamic Biblical Theologizing in Cross Cultural Perspective.* New York. Marry Knoll Orbis.

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Mohamed M.A, na Mohamed, S.A (1998) *Kamusi ya Visawe*. Nairobi. East Africa Educational Publishers.

Mwansoko, H.J.M (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu* Dares - salaam TUKI.

Nanda, S. (1980) *Cultural Anthropology*. California . Litton Educational Publishing.

Neff. D. (2002) *Christianity Today. Meaningful Translation* Interview given by Eugene Nida 7th October 2002 vol.46 No 11

Newmark, P. (1988) *A text Book of Translation.* London. Prentice Hall.

_____(1982) *Approaches to Translation.* Pergamon Press

Nida, E.A (1964) *Towards a Science of Translating*. Leben. E.J Brill.

_____(1969)*The Theory and Practice of Translation*.New York. United Bible Societies

Palmer, F.R (1976) *Semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Payne, R. (1971)*On the Impossibility of Translation,The World of Translation*. New York.PEN.

Pen, J. (1972) *Linguistic Relativity Versus Inate Ideas*. Paris: Mouton.

Petersen, D. (2004)*Translation Journal and the Author.His Excellency and his interpreter*.http://accurapid.com/journal/28 president.htm 30/09/2005

_____(2005)*Translation and the author Source language versus target language bias*. http://www.proz.com/translation articles.30/09/ 2005

Robinson D. (2003) *Becoming a Translator: An Introduction to the Theory and Practice of translation.*Routledge,Taylor and Francis Books LTD

Robinson, C. (1993) *Real World Research: A resource for Social Scientists and Practitioner Researhers*. Oxford. Blackwell Publishers.

Savory T.L. (1975*) The Art of Translation*: London: Jonathan Cape.

Semakula P.S (2000) *Guidelines to Qualitative Research.* Kampala. Uganda National Institute of Special Education.

Shaw R.D (1998) *Transculturation: The cultural Factor in Translation and other communication tasks*.Passadena. William Carey Library.

Shi. A. (2004) *Translation Journal Vol. 8, No. 3* July 2004 Accommodation in Translation.

The Bible Society in East Africa(1968)*The Bible in Luo.* BFBS

United Bible Societies(1952)*Holy Bible in Kiswahili* Union Version.New York UBS

TUKI (1998) *Kamusi Sanifu ya Isimu ya Lugha:* Dares-salaam. Educational Publishers and . . . Distributors.

_____ (1996) *Matumizi ya Kiswahili Bungeni* Dares-salaam: TUKI.

_____ (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dares-salaam: Oxford University Press.

Wendland, E. R. (1987*). The Cultural Factor in Bible Translation.* U.B.S Monograph Series, No.2 New York. United Bible Societies.

**VIAMBATISHO**
**KIAMBATISHO A- TUNUKUZI**

KANDA YA 1

| KIINGEREZA | DHOLUO |
|---|---|
| *K1-1My name is Blaine Rogers. It is a blessing to come to Kenya and again to come to Bondo and see what Jesus is doing in Bondo. I can sense there is a wonderful thing. I am so glad to hear that there are many Christian churches working together for the greatness of God. Amen.* | *Nyinge en……Gweth mathoth biro e Kenya, kendo nyaka Bondo, kendo une gima Yesu timo Bondo. Anyalo neno ni nitie kanise mathoth matiyo kanyachiel, kuom duong' mar Nyasaye. Amen.* |
| *K1-2I want you to know what God is doing all over the world, in the very city that I live in America, 18 churches are coming together, much to built the kingdom, but to build the kingdom of God. Amen! Amen!* | *Adwaro mondo ung'e gigo ma Nyasaye timo e piny duto, ei dala no ma adakie ei Amerika. Kanise apar gaboro biro kanyachiel mondo giger piny ruodh polo mar Nyasaye. Amen.* |
| *K1-3I love to travel, I love to go to places, do I love them? Was I born for this? I was born for this. You don't know the excitements that I experience.* | *Ahero wuotho, kendo ahero dhi kuonde mopogre opogre, be ahero gi? Be nonyuola nigin? Ne onyoula nigin. Ok ung'eyo mor ma asiko ka ango.* |
| *K1-4As I walked into the airport in Nairobi and I walked up, there was a man standing there, and he was waiting to see my passport and my visa. That I had a passport and I had a visa. Amen.* | *Kane adhi e paw ndege ma Nairobi, ne nitie ng'at moro manochung' kanyo, kendo ne orito neno passport na, gi visa mara bende, ka be ne antie gi passport kendo gi visa. Amen* |
| *K1-5As I knew here that I was gonna get come to see you, yes, so he opened it , and he is looking at my visa to Kenya and he got strange look at his face and he said, "you don't have a visa," yes I have it, it is in there, and as he looked, he got it and everything was okay.* | *Kaka ne ang'eyo ni kaye nyaka to abi, ee, noyawo iye kendo ne ongiyo visa mara madhigo Kenya, eka lela wang'e nolokore, mi nowacho kama, ionge gi visa, ee an kode, en eiye kacha, to kane ong'iye, ne oyudo mi oyie ni gikmoko ni kare.* |
| *K1-6He looked at it and signed it then handed it to me, "Have a wonderful time in Kenya" he said, you know what even got into my heart, some years ago.* | *Ne ong'iye mi oketo seyi kuome, bange to nomiya go, ae to owachona kama, "bed gikinde maber ei Kenya" ingeyo gino manosedongo ei chunya higni moko mokadhogo.* |
| *K1-7The Spirit of the Living God began speaking to me, He began to reach down into me, and He began to draw me into Himself. I had no idea where I was going. I did not understand what was happening, but He was helping feel out the possible.* | *Roho mar Nyasaye nochako wuoyo koda, nochako chopo machiegni kuoma, kendo nochako chwala machiegni ire. Ne aonge paro moro, amora, kame ne adhiye. Ok ne anyal ng'eyo, gi manetimore, to notemo kelona gi manyalore.* |

| | |
|---|---|
| *K1-8He began to work in me, He said to me "you were not created for this world.....you were created for the next world." And so He wanted to know the part I wanted that passport for.* | *Nochako tiyo koda, nowachona niya "....ok ne ochweyi nikech pinyni, to ne ochweyi ni piny machielo, kendo nodwaro ng'eyo kama ne adwaro ni passport no."* |
| *K1-9He said, " I went to the cross on the hill, died on the cross, so that you can have a passport." And I thanked Him and I thanked Him, I wanted it I thought in my course might be something. And I wasn't sure that I wanted to pay Him anything. And He kept loving me. And he said, Blaine is that your name? "I already have paid the price"of the Passport for you. And when I realized, it was real that He will give me a passport, I thank God. Amen.* | *Ne awachona niya, "ne adhi e musalaba ewi got, atho e bawo, mondo ibed gi passport," to ne adwokone erokamano, kendo ne agoyo ne erokamano. Ne adware, kendo ne agalonikinde na ne nitie gimoro. To ne osiko ka ohera, eka nowachona niya, "Blaine, mano en nyingi? Asechulo gowi mar passport." To kane aparo ne en adiera, ni obiro miya passport. Ne agone Nyasaye erokamano. Amen.* |
| *K1-10 I have a passport to next world, how many have a passport? Are you getting ready? You are getting excited. I am excited as I travel, Amen.* | *Antie gi otiko mar piny machielo, ji adi man gi passport? Be uikore? Amor ero lombo u. asiko ka amor seche ma awuotho. Amen.* |
| *K1-11 What about visa? We have got to have visa too including passport. We must have visa. My visa is being made. And I've got good news, your visa is being made too. Halleluyah. If you are having a bible I want you to open with me Mathew 22* | *En ang'o kuo visa? Onego wabed gi visa kaachiel gi passport, nyaka wabed gi visa. Visa ni iloso, kendo an gi weche manyien kuomu, ni visa maru bende iloso. Halleluya. Ka untie gi mumbeu, el uru koda kaachiel, Mathayo 22.* |
| *K1-12 I'll go a little slow as we do in America. See this lovely flower right here, flower can you rise up, this is my lovely wife. Ah I can see you, thank you.* | *Abiro dhi mamos to ok ahinya kak watimo ei Amerika. Ng'i uru mauwa maber man ka ni, mauwa chung' ane malo, ma en jaoda mahero, to kendo anyalo, neni., erokamano.* |
| *K1-13 Judy's grandmother she came from a country called Ireland. She was born in Ireland. When she was 16-17 her great grandmother took her grandmother and placed them in a boat and kissed them and said to them goodbye.* | *Dan Judi, ne owuok e piny miluongo ni Ireland, ne onyuole Ireland. To kane ojahigni maromo 16 kata 17, dangi maduong nokawo dangi, moketo gi ei yie, bang'e to nonyodho gi seche mane ogongi oriti.* |

| | |
|---|---|
| *K1-14And sent them to America; she wanted to get them out of Ireland. And have them come to America to start a new life. My wife is a product of years later and I met the flower of my life. We married and I went to meet her grandmother, would you do that? To meet the grandmother. It was an experience.* | *Kendo ne ooro gi Amerika, ne odwaro mondo ogolgi oko mar Ireland. Kendo ne odwaro ni gibi Amerika mondo gichak ngima manyien kuno. To jaoda ne olemo mar higni moko mabang'e go, kendo ne aromo gi mauwa ma mar ngima na. Ne wakendore kendo nadhi mondo arom gi dan mare. Be inyalo timo mano, romo gi dangi. Ne en gima atimo.* |
| *K1-15She lived on one side of America we lived the other side of America, I thought I was safe. So I would have to meet the grandma, so when she was visiting, I really cherished the chance to meet her. I had to sit down and talk and the first thing she said to me "I was born a catholic I gonna die a catholic, okay"* | *Ne odak loka machielo mar Amerika, to wan be wadak bathe komachielo mar Amerika. Ne aparo ni apondo, to kane obiro limbe, ne adhialo ahinya thuolo no mar romo kode, ne nyaka abed piny mi awuo, to gima okuongo manowachona, "ne onyuola ei katholik, kendo an atho jakatholik, O.K"* |
| *K1-16I'm Blaine, I had met you. She was a little vexed at me because my wife had grown up as a Catholic. But along the way God intervened and she got born again. I thought it was my fault and I knew that right away* | *An Blaine, aseromo kodi. Ne abwok ahinya koda nikech jaoda ne odak ka en jakatholik, to bang'e, Nyasaye nofwenyore ne, minoyudo warruok. Ne aparo ni en wachna, ne ang'eyo mana kamano* |
| *K1-17 What was amazing to me is how some people label themselves, I am a catholic, I am a Baptist or I am an Anglican or I am a Presbyterian, Amen.* | *Mano nokawa gi paro ahinya kaka jomoko chakore kendo luongore ni jakatholik, ne otisa, an ja Anglikan, an ja Presbyterian. Amen* |
| *K1-18 Im going to read first for you, would we go to Mathew 22:34 "when the Pharisees heard that"* | *Adhi somo nu mondi, we wadhi uru e Mathayo 22 kwan matindo 34, kane jo farisai owinjo wachno* |
| *K1-19You shall love Lord your God with all your heart, with all your soul, with all your mind. This is the first and the great commandment and the second is like this, you shall love your neighbour as yourself and on these two commandments and all the law and the prophets. This was the answer that Jesus gave.* | *Owinjore uher Nyasaye manyasachu, gi chunyu duto, kendogi roho u duto, gi pachu duto. Mae chik mokwongo kendo e maduongie, to mar ariyo chalo kama, in iher jawadu kaka iherori iwuon, kendo kuom chike ariyogi kod chik duto kod kor duto. Ma e ang'sa mane Yesu ochiwo* |
| *K1-20 As he was preparing to demonstrate His great love for man, He did know that solely He's going to have to hung on the cross that he was going to demonstrate the greatest of love* | *Kaka ne oikore mondo onyis herane mogundho ni dhano, Ne ong'eyo ni to adiera odhi dere ebao, kendo ni odhi dere emusalaba, mondo onyiswa go herane mogundhono.* |

| | |
|---|---|
| *K1-21 That Jesus had to completely pour Himself out for you and I. He did not surely need a level. He was going live where he had lived. So many times I 'll ask the world " what do you mean " love with all your heart and all your mind and all your soul? Because I thought that Jesus meant something special* | *Onego odhi ochiwre te ni in kendo ni an. Ok ne odich gi ranyisi, Ne odhi dala kama ne osebedo kodakie seche mathoth, abiro penjo piny. Ere tiend wach mar hero gi chunyi, kendo gi rohoni? Nikech aparo ni Yesu nomino gimoro makende.* |
| *K1-22 And so as I live my life I experience the trials of life. He began to show me; I would be in a situation where somebody would comfort me. Could any kind of situation. And I will begin to respond for me and who I am and to Jesus and the Holy Spirit.* | *Kendo kaka adak engima na, e tembe mathoth engima, gigo mabeyo kendo maricho engima. Ne osechako nyisa ni nabed ekinde moro ma ng'at machielo emohoya, onyalo kinde moro amora. Kendo abiro chako chiwra awuon kendo ni ng'ama an kendo ni Yesu Kristo to gi roho maler* |
| *K1-23 Will you stand and say " love thy God with all thy heart, mind, might and all thy soul. And then I will stand and say "Lord... live in me, you love me let me respond in loving you." That is not always an easy thing.* | *An achung' mi awachi ni her Nyasachi gi chunyi duto gi paroni duto kendo an achung' mi awach ni Ruodha, dag kuoma", ni hera, we achiwra e heri, mano ok osebedo gimayot.* |
| *K1-24 So I didn't realize that when He is wanting me to love Him. As a man that was what I was going to learn how He loved me so that I could also return that love to others. He said to love your neighbour as yourself. What does that mean? When it's hard to do.* | *Omiyo ne ok anyal paro ni kane odwara ni mondo ahere, kaka dichuo ni ne adhi somo kaka ne ohera, mondo aduog mialam jomoko bende. Ne owacho ni her nyawadu kaka iherori in iwuon, Mano tiende en ango? Ka otek timo.* |
| *K1-25 This February my lovely flower and I celebrate 30 years marriage together. Isn't that a miracle? Actually a miracle of God because without the love of Jesus in me, she would never put up with me but Jesus would come to me and break me not to hurt me but to say love her.....love her.....love her. I told Him my God I'm trying.....trying. And He said "you have not tried it enough " but God "I'm right! She is wrong!" and he said you've not tried hard enough. love me .....I'll help you love her.* | *Ei February ka, maupa majaber kod an riwre enyasi mar higni 30 mar kend, Be mano en hono? Adiera hono mar Nyasaye. Nikech kaonge hera mar Yesu kuoma to ne ok onyal dak koda, to Yesu ne nyalo biro kuoma, kendo otura piny, ok no hinya, to mana wacho ni here, here. Ne anyise ni Nyasacha atemo to no nyisa ni pok itemo moromo, to Nyasaye an kare, to en ema okoso, to nowacho niya, pok itemo ahinya moromo, hera... abiro konyi here.* |
| *K1-26 I had to do the right steps. It's that step one and this is step two. First love me then you can love her. You see I really watch from above who is wrong* | *Nyaka atim mana gimakare, en ondamo no kendo gi ondamo mar hera, bang'e to inyalo here, Ine ni ber asiko ka arango koa malo, ng'ama ni kare gi ng'ama ok ni kare. Yesu* |

| | |
|---|---|
| *and who is right. Jesus said about true love first is not that who will stand in the judgment first is not that who will be critical first. Even though I'm a little slow the light began to come on.* | *nowacho kuom hera mar adiera ni ok en ng'ama nobi nyim jang'ad bura mokwongo ok en ng'ama nonon matut, Ng'ama noher mokwongo. Kata odoko ni adhi mos, ler osechako biro machiegni.* |
| *K1-27 I began to understand when I was wrong to Jesus. How many know we can be wrong to Jesus? He just loved me, He will love me. He will say, "yes you are wrong but I love you my blood I shed at Calvary. It redeemed you. I love you it's okay." But I didn't feel it was okay. I had the feelings those are the kinds of things that makes us label ourselves.* | *Ne achako ng'eyo kama ne okoso enyim Yesu, ne ohera ahera, to pod obiro hera. Obiro wacho ni ee nikoso, to mak mana ni aheri, remba ne ochwer kalvari, ni owari, aheri to ok ne awinjo ni kane an gi paro ni mago gin gigo ma miyowa chakre nying.* |
| *K1-28 And God was saying "No.... I love you .Hey!" and when I felt that love then I would respond to it back and everything would be okay. How is it? That Christian brother with all this different labels. Could ever work together is because when Jesus comes to them. And He says to love them then they love. That is what is working. Isn't that a good thing?* | *To Nyasaye ne wacho ni da, ok en kaka iparo no, aheri ei yo kane awinjo herano, to ne anyalo duoko mi gik moko nobed kare, En nang'o? Ni owete jokristo, gi ranyisi?kido mopogre opogre gi, nyalo tiyo kamaro achiel, nikech Yesu nobiro negi. Kendo osingo herogi kaka giherore. Mano e gima tiyo, mano ok en gima ber ?* |
| *K1-29 There is a dying world that desperately needs the same love that I have experienced in my life. It is the same love that I have experienced, that you have experienced in your life. How many here do that saying "I know what you are talking about" what do you mean? Because I love Jesus that is in me. Wave at me ..... Amen! You know the love of Jesus is in your life.* | *Nitie piny matho modich gi hera nogono, ma ni. en heranogo no, maise yudo engimani. Ji adi ka matimo kamano ang'eyo gima iwuoyo kuome, tiende en ango? Nikech ang'eyo herano mar Yesu man kuoma no. Fwa na uru...Amen. Ing'eyo hera mar Yesu man kuomi no.* |
| *K1-30 And we needed it when we found it when Jesus came to us it passed on the cross, we needed it. We need it today, we need it tonight, we need it tomorrow and we will need it next day. Because it is the visa of heaven so we have no choice in heaven. We have to love each other. So we need to love each. So we need to heed to it now. I want to love this woman; not just of today and tomorrow. Not just to work this far but to eternity to next world too. So I need to learn to love her today.* | *To ne wadich kode, kane Yesu obironwa, to ne okalo kuom msalaba, wadich kode. Wadich kode kawuono, wadich kode gotieno, wadich kode kiny, kendo wabiro dich kode ei seche mabirogo nikech en visa mar polo, omiyo wangie yiero e polo, nyaka waher jowadwa. Koro onego wakane sani, adwaro hero dadani, ok hera mag miriambo makawuono gi kiny . Ok ni nyaka wawuoth maber kuomi, to nyaka epiny machielo no bee, koro puonjri here kawuono, onego wapuonjre hero ngato.* |

| | |
|---|---|
| *K1-31 Does ever one wake up at night and see the sky? See all the stars, see all the light, see all the beauty. I wonder what gonna be life. Before we get to see it. So it would be wonderful. It gonna be the greatest thing because it's going to be next life, all you are going to experience from the top of being to the bottom of our being completely in the truth of love.* | *Be ng'ato nyalo chiew gotieno mi one polo? One sulwe duto, one ler duto, one ber mi owuor gima ngima en kapok wachopo ma wane ni ober. Odhi bedo gino maduong'I e moloyo nikech odhi bedo ngima manyien, gima wan duto wadhi , koa malo nyaka piny marwa obedo mogik kuom adiera mar hera.* |
| *K1-32 Colossians 3:14. here the apostle is writing to the church of Colossians. He is talking to them about new man and the cloth the new man needs to put on. It's a character of tenderness, kindness, humility and meekness and long suffering. But he did say, "put on love" so love is what brings us to perfection. It is the bond of perfection. All these other things work in us and they are wonderful things. As I come to Africa, one thing I notice Christians here are so fine, nice, treat us with such a respect, reverence and I'm so greatly appreciating we thank you so much.* | *Jo Kolosai 3:14 Kae janabi ndiko ni Kanisa mar jokolosai kowuoyo kuom ng'at manyien gi law ma ngat manyien onego rwaki, en ranyisi mar ng'wono mohore, bebo ratiro, kendo bedo maonge mibadhi. To nowacho, rwak hera, omiyo hera e gino ma keto wa kare, en yie ratiro mar bedo kare, Gik moko machielo go man kuomwa go to be beyo. Kane abiro Africa, gima awuoro , en ni Jokristo man ka ni kare, beyo, omiyo wa luor gi dhial, omiyo amor ahinya , agoyo erokamano, ahinya.* |
| *K1-33 He wants us to go beyond. He wants us to truly love each other. He wants us to go all the way to the wholeness of what love is. And the only one that which teaches is Jesus. Because He has complete love. Do you want Him to teach you love? Do you want Him to work that in your life for the completeness and perfection for Christ to work in you. He wants to do that in every one. Amen!* | *Odwaro wa mondo wadhi mbele gima ni mbele wa lo, hera mar adier ni jowetewa. Odwaro ni mondo wadhi kuonde go te kaachiel kuom gima hera en. To ng'ato kende manopuonjwa en Yesu, nikech en gi hera mopong'. Be idwaro ni mondo opuonji hera? Be idwara ni oti gino man kuomino, mopange gi adiera gi ratiro mar Jakristo mondo oti kuomu. Odwaro timo kamano ni ji te. Amen.* |
| *K1-34 Why do I do, what I do?*<br>*Answer*<br>*All we should do we should do because of Jesus*<br>*Because of Jesus* | *En ang'o momiyo atimo gima atimo? En ang'o. Ang'sa, gik moko duto watimo nikech Yesu, nikech Yesu.* |
| *K1-35 Because I'm gonna respond to the first command and I'm gonna love the word that God with all my heart and all my heart and all my soul and that I have that He has to be reason for all.* | *Nikech adhi dwoko chik mokwongono, adhi hero Nyasaye moloyo piny gi chunya duto, gi gigo duto ma an go ma ase bedo nikech gik moko duto.* |

KANDA YA 2

| KIINGEREZA | DHOLUO |
|---|---|
| *K2-1 .....Love..... it doesn't matter whether from America, from Bondo, from Uganda. It doesn't matter we have the same spirit. That God has infused into us Amen! And God desires that we should be one. That we should know equally. And what I know and you know be put together. This is why we have the privilege of preaching to you and listening as you preach. I feel the love of God as you began to worship and sing and wave my hands with you. I felt the presence of God, the power of God and he was working through you. He has established because He desires that we should know His ways.* | *Hera, ok lich kata kia Amerika,kata Bondo, kata Uganda. Ok ochuno, wan gi roho achiel ma Nyasaye oseketonwa. Amen. Kendo Nyasaye dwaro mondo wabed gachiel. Mondo wang'e marom, to gima wang'eyo, ni onego ket kamoro achiel, ma e momiyo wan gi thuolo ni makende mar lamo kanyachiel. Mamiyo wan gi thuolo mar yalo ni kendo winjo kaka uyalo. Awinjo hera mar Nyasaye, kaka nuchako lemo kendo wer kendo fwayo lweta kodu. Awinjo bedo machiegni mar Nyasaye, teko mar Nyasaye, kendo kanotiyo kokalo kuomu, oseketo gombo mar ng'eyo yorene.* |
